Jumamosi Novemba 4, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0581484
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US




**Madaktari** waliofeli kurudia mitihani

UKURASA 2



**Mapya** yaibuka gari linalodaiwa kutumika mauaji dada bilionea

UKURASA 4

**Israel** yazidisha mashambulizi Ukanda wa Gaza

UKURASA 17

**MADRID YAANIKA DAU KUMNASA VINICIUS JR**

UKURASA 21

## RIPOTI YA CAG:

# Wabunge wataka vigogo wanyongwe

• **NI** waliotajwa tuhuma za ubadhirifu mabilioni , wataka sheria kutungwa... *Ukurasa 2*



**"Hatua ya kwanza ya kuondokana na vitendo vya ufisadi ni CCM kujitenga na watu hao. Wanaohusika waondolewe na kuwaweka watu wengine wenye hofu ya kuiba." – Ole Sendeka.**

**"Mimi nilitarajia watuambie baada ya ripoti ya CAG wangapi wamefungwa? Wangapi wamefikishwa mahakamani? ... Pendekezo pekee iletwe sheria hapa watakaokutwa na hatia wanyongwe." – Mwita Waitara.**





**"Wahusika wote waliotajwa katika ripoti ya CAG wapelekwe gerezani na wakafanye kazi za kulima hadi watakaporejesha fedha walizoiba." – Joseph Kasheku.**




Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni ya Three Road Co. Ltd, Dingcheng Li (kulia), akionyesha kwa waandishi wa habari uharibifu mkubwa uliofanywa baada ya kuvamiwa na kundi la zaidi ya watu 50 katika ofisi za kampuni hiyo, Mikocheni Viwandani, Kinondoni mkoani Dar es Salaam jana na kuibwa vifaa mbalimbali zikiwamo kompyuta, simu na fedha taslimu zaidi ya Sh. milioni 23 na Dola za Kimarekani 25, 000. **PICHA: JOHN BADI**

## Mkuu wa shule akatwa mapanga wakati akisimamia ujenzi wa shule kwa walimu

UKURASA 4

# PAC yabaini kasoro ujenzi reli SGR

UK. 3

**MICHEZO** **ROBERTINHO, GAMONDI USHINDI 100%** UK.24 **MAONI** UK.6



Rais Samia Suluhu Hassan akipokea Ujumbe Maalum kutoka kwa Mfalme wa Saudi Arabia, Salman bin Abdulazizi Al Saud uliowasilishwa na Balozi wa Saudi Arabia hapa nchini Yahya Ahmed Okesh, Ikulu jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

# Wabunge wataka vigogo ripoti CAG wanyongwe, wakatwe vichwa

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

WABUNGE wametoa mapendekezo ya kunyongwa au kukatwa vichwa kwa viongozi wa serikali wakiwamo mawaziri na watumishi wa umma waliotajwa kuhusika na ufujaji wa fedha katika ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

Wamesema ni wakati muafaka wa kuwasilishwa bungeni muswada na kutungwa sheria ya kutekeleza jambo hilo ili iwe fundisho kwa watu wengine wenye tabia ya udokozi wa fedha za umma.

Mbunge wa Tarime Vijijini (CCM), Mwita Waitara, alisema ameshuhudia taarifa za CAG kwa zaidi ya miaka mitatu akiwa bungeni lakini hakuna hatua zozote zilizochukuliwa dhidi ya wahusika wanaotajwa kuhusika na ubadhirifu.

Alisema kasi ya Rais Samia Suluhu Hassan kutafuta fedha ni kubwa lakini pia kasi ya wizi wa fedha za umma imekua kubwa sana.

Mwita alisema hatua hiyo ni sawa na Rais Samia anachota maji anaweka kwenye mkono wa kushoto lakini kuna watu wanatoboa pakacha, hivyo hayo maji hayawezi kujaa.

"Na mimi ninamapendekezo yangu, nchi kama Korea watu wanaokutwa na hatia ya ufisadi wananyongwa, sasa ninapendekeza waliodhibitika pasipo shaka bila ya kuwaonea wanyongwe, watoke katika nchi hii tubaki na watu wema," alisema Waitara.

Alisema Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) imetoa mapendekezo mazuri, lakini yamepungua uzito.

"Mimi nilitarajia watuambie baada ya ripoti ya CAG wangapi wamefungwa? Wangapi wamefikishwa mahakamani? Wangapi wamefukuzwa kazi? wangapi wamerudisha fedha?. Pendekezo pekee ni kwamba iletwe sheria hapa watakaokutwa na hatia wanyongwe," alisisitiza.

Mbunge wa Mbog'hwe (CCM), Nicodemus Maganga, aliunga mkono kuwapo kwa sheria ya kunyongwa kwa viongozi watakaobainika kuhusika katika ufujaji wa fedha ili kukomesha tabia hiyo.

"Ninaungana na (Mheshimiwa) Mwita kwenye sheria ya kunyongwa. Tuipitishe hii sheria ili tuondokane na hii kitu. Kwa zaidi ya miaka mitatu nimekuwa nikiongelea suala hili, sasa ni wakati muafaka," alisema Maganga.

Naye Mbunge wa Makambako (CCM), Deo Sanga, alisema: "Kupitishwa kwa sheria ya kunyongwa kwa viongozi watakaobainika na ufisadi, itapunguza tabia ya watu kuiba. Sheria iletwe hapa bungeni itasaidia watu kuogopa kuiba."

Mbunge wa Simanjiro (CCM), Christopher Ole-Sendeka, alisema hatua ya kwanza ya kuondokana na vitendo vya ufisadi ni Chama Cha Mapinduzi (CCM) kujitenga na watu hao.

Alisema mawaziri wanapaswa kujitenga na maofisa wanaohusika katika ufisadi kwa kuwaondoa na kuwaweka watu wengine ambao wanahofu ya kuiba. Mbunge wa Kigoma Mjini (CCM), Kilumbe Ng'enda, alisema matukio ya watu kufanya ubadhirifu wa fedha za umma yanaongezeka kila mwaka, hivyo ni wakati muafaka wa serikali kuleta muswada bungeni na kutungwa kwa sheria ya kunyongwa kwa watu hao au hata ikiwekezana kukatwa kichwa.

Mbunge wa Liwale (CCM), Zuberi Kuchauka, aliunga mkono hoja ya kutungwa kwa sheria kali ya kudhibiti vitendo vya ufujaji wa fedha, akisema itungwe ili iwe fundisho.

**MBARAWA, NCHEMBA, WATAJWA**

Mbunge wa Kisesa (CCM), Luhaga Mpina, alipendekeza Waziri wa Uchukuzi, Makame Mbarawa, Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania (TRC), Masanja Kadogosa, wakamatwe na kushtakiwa kwa makosa ya uhujumu uchumi.

Mbunge wa Geita (CCM), Joseph Kasheku, alipendekeza wahusika wote waliotajwa katika ripoti ya CAG wapelekwe gerezani na wakafanye kazi za kulima hadi watakaporejesha fedha walizoiba.

# Madaktari waliofeli kurudia mtihani

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Afya, Ummy Mwalimu, ameagiza madaktari tarajali wote waliofeli mitihani iliyoandaliwa na Baraza la Madaktari Tanganyika (MCT) kurudia.

Ummy alisema hayo jana jijini hapa, wakati akipokea ripoti ya tume huru ya uchunguzi wa malalamiko ya madaktari hao iliyoongozwa na Mwenyekiti wake, Prof. Mohammed Bakari Kambi.

Alisema ripoti iliyotolewa na tume hiyo imebaini kuwa malalamiko yaliyotolewa na madaktari hao hayana mashiko kwa kuwa uchunguzi umebaini hakuna aliyeonewa wala kupendelewa.

"Ndugu wanahabari, mtakumbuka kuwa niliunda tume hii mara baada ya kupokea barua ya malalamiko ya madaktari tarajali ambayo iliandikwa na kupelekwa kwa Mheshimiwa Rais na nakala nikapatiwa mimi.

"Tume hii imekamilisha uchunguzi wake na kubaini kuwa, wale ambao walifeli katika mitihani ile, walifeli kihalali na hakuna kuonewa kama ambavyo walivyokuwa wakilalamika katika barua yao," alisema.

Waziri Ummy alisema kwa mujibu wa tume hiyo ambayo iliongozwa na Prof. Mohammed Kambi, aliyewahi kuwa Mganga Mkuu wa Serikali, ilifanya uchunguzi kwa kuhoji wadau mbalimbali.

Alisema licha ya kuhoji wadau mbalimbali, lakini pia ilipitia mitihani hiyo na kusahihisha upya na kubaini kuwa, wale waliofeli matokeo yalikuwa sahihi na hawakuonewa.

"Ninaagiza wote waolifeli warudie mtihani kwani sheria inawaruhusu kufanya mara tatu na atakayefeli awamu zote itabidi akasome upya mafunzo tarajali kwa miezi sita," alisema.

Waziri Ummy aliagiza MCT kuendelea kuandaa mitihani hiyo kwa mujibu wa sheria.

Alisema lengo la mitihani hiyo ni kupima uwezo wa madaktari tarajali kabla kupatiwa leseni za kutoa huduma.

"Ninakubaliana na mapendekezo ya tume kuwa, mtihani huu ni jambo la muhimu sana ili kupata wataalam ambao watatoa huduma zisizokuwa na mashaka au malalamiko kwa jamii," alisema.

Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel, alisema pamoja na uwapo wa mtihani huo, kuna haja kufanyika ukaguzi kwa vyuo vinavyotoa wataalam wa afya.

"Kwenye taaluma ya afya makosa hayaruhusiwi, ukimkosea kumtibu mtu unampa tiketi ya kifo au ulemavu wa kudumu tofauti nakada zingine kama sheria, mtu anaweza kukataa rufani," alisema.

Mwenyekiti wa Tume hiyo, Prof. Kambi, alisema uchunguzi wa ripoti hiyo umefanyika kwa muda wa wiki tatu kwa kuhoji wadau mbalimbali wakiwamo walalamikaji na wasimamizi wa mitihani.

"Tulipatiwa wiki mbili kwa ajili ya kufanya uchunguzi lakini kutokana na ukubwa wa kazi hii tuliongeza muda wa wiki moja ambapo tulihoji wadau mbalimbali, kuandaa madodoso na kuhoji kwa njia ya mitandao kwa wale waliokuwa mbali," alisema.

HABARI KITAIFA



Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye (kulia), akimsikiliza Mbunge wa Vunjo, Dk. Charles Kimei, bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# PAC yabaini kasoro mradi ujenzi SGR

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

KAMATI ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) imebaini kasoro katika ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR), zikiwamo ununuzi, kuchelewa kukamilika kwa mradi na gharama za mradi wenyewe.

Akiwasilisha bungeni kuhusu ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) , Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Japhet Hasunga, alisema ukaguzi wa kiufundi ulizingatia vipande vitano vya mradi.

Alivitaja vipande hivyo ni ni kipande cha kwanza na cha pili (Dar es Salaam hadi Morogoro; na Morogoro hadi Makutupora) ambao ulilenga kufuatilia mapendekezo ya ukaguzi wa awali, kazi ambazo hazijakamilika, uwekaji wa mfumo wa umeme, ununuzi wa mabehewa na vichwa vya kuvuta mabehewa na ufungaji wa ishara na mawasiliano.

Hasunga alisema kwa vipande vya tatum nne na tano, ukaguzi ulijikita kwenye hatua zote za mradi ikihusisha kupanga mradi, usanifu wa awali, mchakato wa ununuzi wa mkandarasi, utekelezaji wa mkataba na kufuatilia kuzingatiwa kwa masuala ya rasilimali watu, mazingira, usalama kazini, na mambo ya kijamii.

UNUNUZI VICHWA, MABEHEWA

Hasunga alisema katika mchakato wa ununuzi wa mabehewa ya treni, taarifa ya ukaguzi wa kiufundi imebainisha upungufu mbalimbali.

Alisema kwanza TRC ilikataa zabuni mara mbili kwa ajili ya ununuzi wa vichwa vya treni ya umeme na makochi na mabehewa ya abiria. Mzabuni aliye na bei ya Dola za Marekani 263,460,514 alikataliwa na kufanya ununuzi usio na ushindani kwa Dola za Marekani 478,507,468 kulikosababisha ongezeko la gharama ya Dola za Marekani 215,046,954 (sawa na ongezeko la asilimia 82) lisilo la lazima.

Hasunga alisema katika mkataba wa ununuzi wa makochi na mabehewa ya abiria yaliyotumika, TRC ilitekeleza mkataba bila dhamana ya utendaji kazi, hali iliyosababisha hasara ya Euro 5,320,400 (Sh. bilioni 13.7).

Alisema alisema TRC ilimwomba Balozi wa Tanzania nchini Uturuki kufanya uchunguzi wa kina kwa mzabuni M/s Eurowagon juu ya ununuzi wa vichwa viwili na mabehewa 30 ya abiria yaliyotumika ili kuthibitisha hali ya kisheria na uwapo wa kampuni, uwezo wa kitaalamu na kiufundi, uwezo wa rasilimali na uthibitishaji wa wateja wanaohudumiwa au waliowahi kufanya kazi na kampuni hiyo. Alisema katika uchunguzi huo, balozi alibaini kuwa kampuni haitekelezi mradi wowote unaoendana na huo kwa sasa.

Pia alisema uwezo wa kifedha wa kampuni ulibainika kutotosha kutekeleza mradi wa uingizaji wa mabehewa yaliyotumika nchini isipokuwa walipata ufadhili kutoka kwa vyanzo vingine.

Hasunga alisema licha ya upungufu hayo yaliyobainishwa na balozi, bado TRC iliidhinisha zabuni hiyo kutolewa kwa M/s Eurowagon.

Aidha, Hasunga alisema kampuni ya M/s Eurowagon haikuwasilisha dhamana ya utendajikazi licha ya kukumbushwa mara kadhaa na TRC.

Alisema TRC iliendelea kutekeleza mkataba huu pasipo kupatiwa dhamana ya utendajikazi jambo ambalo lilisababisha kusitishwa kwa mkataba pasipo kukata dhamana kama fidia kwa kutotimiza wajibu wa kazi.

"Zaidi ya hayo, kifungu kidogo cha 8.7 cha mkataba kati ya TRC na M/S Eurowagon kinaitaka kutoza asilimia 0.15 ya thamani ya mkataba kwa siku kama fidia ya bidhaa ambazo hazijawasilishwa hadi kiwango cha juu cha asilimia 10 ya thamani ya mkataba," alisema Hasunga.

Tano, Hasunga alisema TRC haikutoza Euro 2,660,200 kwa ucheleweshaji wa kuwasilisha bidhaa, hivyo kuleta hasara ya ya Euro 2,660,200 ambayo ingekatwa kama fidia ya dhamana ya utendajikazi na kusababisha hasara ya Euro 5,320,400.

**ONGEZEKO LA GHARAMA**

Hasunga alisema kwa mujibu wa taarifa ya CAG mapitio ya nyaraka za mikataba zilizotolewa kwa vipande vya kwanza, pili na tano, yalibaini uwepo wa ongezeko la gharama za ujenzi wa SGR kwa kilomita.

Alisema taarifa ya ukaguzi inafafanua kwamba kwa vipande kwanza, pili na tano, kwa kutumia njia ya ushindani gharama za ujenzi kwa kilomita moja ilikuwa Dola za Marekani milioni 4.1, milioni 4.6 na milioni 3.9 mtawalia, wakati kwa kipande cha tatui na nne mchakato wa zabuni ulifanyika kwa njia ya mzabuni mmoja, gharama ya ujenzi wa SGR kwa kilomita moja ilikuwa Dola za Marekani milioni 5.2 na Dola milioni 5.5 mtawalia.

Hasunga alisema kutokana na tofauti hiyo, taarifa ya CAG inabainisha kwamba hapakuwa na faida ya kiuchumi kwa Shirika la Reli (TRC) kwa kutoa zabuni kupitia njia ya chanzo kimoja kwa kampui ya M/S Yapi Merkezi.

"Hii ni kwa sababu gharama za awali ujenzi wa miradi mingine zilikuwa chini ikilinganishwa na mkataba aliopewa mkandarasi wa kipande cha nne na tano. Pamoja na hilo, ukaguzi ulibaini kuwa mawanda ya kazi kwa kipande cha 3 na 4 ya mradi yalikuwa madogo na yalikuwa na miundombinu michache kuliko ile ya kipande cha kwanza, pili na tano," alisema.

**ONGEZEKO LA MUDA**

Hasunga alisema kwa mujibu wa mkataba namba PA/003/HQ/2016-17/W/01 wa ujenzi wa SGR kati ya Kampuni Hodhi ya Rasilimali za Reli Tanzania (RAHCO) inayojulikana kwa sasa kama TRC na YAPI-MOTA ENGIL JV, mkataba huo ulitakiwa kukamilika Novemba Mosi, 2019.

Hata hivyo, alisema taarifa ya CAG inabainisha kuwa, mradi huo uliongezwa muda wa kukamilika mara saba, na kuongeza siku 1,414 hadi muda wa kukamilika, sawa na miaka mitatu na miezi tisa.

Hasunga alisema sababu za kuchelewa kulitokana na kuchelewa kwa uamuzi wa uhamishaji wa miundombinu ya bandari na makabidhiano ya eneo la ujenzi na kuchangia kuchelewa kwa mradi kwa siku 959.

Sababu nyingine ni kuchelewa kwa uamuzi kuhusu kiunganishi cha bandari cha kilomita nne na reli ya zamani (MGR), na kuchelewa makabidhiano ya eneo la kazi.

Sababu nyingine ni kuanzishwa kwa njia za juu na mapitio na marekebisho ya mwajiri ya njia ya eneo la 6.1, 9.1, na 11.1, ikijumuisha kuchelewa zaidi kutompa mkandarasi eneo kamili la kazi na uhamishaji wa miundombinu, muda wa umalizaji kazi uliongezwa hadi Septemba 15, mwaka huu.

## Serikali yasisitiza mtoto anayezaliwa hospitalini atumie bima ya mama yake

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imesema kuanzia sasa mtoto anayezaliwa hospitalini ambaye mama yake ana kadi ya bima ya afya atahudumiwa kupitia kadi hiyo.

Hivyo, imewaelekeza watendaji wa mfuko wa bima ya afya na vituo vyote vya huduma za afya kuhakikisha watoto na wazazi hawapati shida kwa kuwa, mama yupo na kadi yake inaonyesha ushahidi wote kuhusu kichanga na ni mtoto ngapi kwenye familia.

Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel, alitoa kauli hiyo bungeni alipokuwa akijibu maswali ya nyongeza ya Mbunge wa Manyoni Magharibi (CCM), Yahaya Masare.

Katika swali lake, Mbunge huyo alihoji katika sheria ya bima ya afya kwa wote iliyopitishwa juzi kama itajumuisha mtoto anayezaliwa kutumia kadi ya bima ya mama ya angalau kwa miezi mitatu wakati mzazi anajipanga kutengeneza bima yake.

Alisema serikali ilishatoa maelekezo mara kadhaa kuhusu mtoto mchanga kutumia bima ya mama yake na kuhoji kauli ya serikali kutokana na jambo hilo kujirudia.

Akijibu swali hilo, Dk. Mollel alisema, "Kuanzia sasa tukisikia suala la mtoto mchanga kutopata matibabu kupitia bima ya mama yake, tutachukua hatua kwa mtu atakayesababisha kikwazo hicho,"alisema.

Awali katika swali la msingi, Mbunge wa Viti maalum (CCM), Martha Gwau, alihoji serikali haioni kuna haja ya watoto wachanga kutumia bima za afya za mama zao.

Dk. Mollel akijibu swali hilo, alikiri kuwapo kwa changamoto kwa wazazi wenye bima wanaojifungua watoto wao kushindwa kupata huduma hasa kwenye vituo vya huduma za afya vya sekta binafsi.

Aidha, alisema Wizara ilishatoa maelekezo kwa Mtendaji Mkuu wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kuhakikisha watoto wachanga wenye uhitaji wa huduma wanapata huduma za afya bila kikwazo chochote.

"Niwaase wazazi na viongozi wa hospitali husika kukomesha kabisa matukio ya kughushi nyaraka ambayo pia ndio yanapelekea kuwepo kwa usumbufu wakati mwingine,"alisema.



Mwalimu Dagau akiwa hospitalini akiwa amelazwa baada ya kukatwa mapanga.
**PICHA: SABATO KASIKA.**

# Mkuu wa shule akatwa mapanga wakati akisimamia ujenzi wa shule

**Na Sabato Kasika**

MKUU wa Shule ya Sekondari Makojo, iliyoko Kijiji cha Makojo, Musoma mkoani Mara, Emmanuel Dagau, amenusurika kifo baada ya kucharangwa mapanga na mkazi wa kijiji hicho, Jaguji Musimo, akimtuhumu kuharibu eneo lake la kuchimba mchanga.

Mwenyekiti wa Kijiji hicho, Julius Misana, akizungumza na mwandishi wa habari hii kwa njia ya simu jana, alisema tukio lilitokea Jumatano, saa nane mchana, wakati mwalimu huyo akisimamia ujenzi wa bweni la shule yake.

Mwenyekiti huyo alisema mtuhumiwa anashikiliwa na vyombo vya dola, huku mwalimu akiwa amelazwa katika hospitali ya rufani ya Mwalimu Nyerere iliyopo mjini Musoma.

"Siku ya tukio mwalimu alikuwa anasimamia wanafunzi kusomba mchanga kwa ajili ya ujenzi wa bweni, lakini (mtuhumiwa) akadai kuwa ni kwenye eneo lake. Ndipo baadaye akamfuata mwalimu nyumbani kwake na kuanza kumshambulia kwa panga," alisema.

Alisema wanafunzi walioshuhudia tukio hilo, walipiga kelele na (mtuhumiwa) akakimbia lakini polisi waliokuwa wakisimamia mtihani shuleni hapo walipopata taarifa walimfuatilia na kumkamata.

"Amefanya kitendo cha kutia doa kijiji chetu na kusababisha walimu kuogopa kuja kufundisha katika shule yetu wakihofia maisha yao," alisema.

Misana alisema mtuhumiwa huyo amemjeruhi mwalimu huyo sehemu mbalimbali za mwili ikiwamo na mikono na kumsababishia majeraha makubwa.

Mwenyekiti huyo alikanusha ya madai wanafunzi kuchota mchanga katika eneo mtuhumiwa kwa kuwa baada ya taarifa za tukio alifika kujiridhisha na kukuta sivyo kama alivyodai.

Mbunge wa Musoma Vijijini, Profesa Sospeter Muhongo, alisema kumekuwapo mtindo wa baadhi ya madiwani na wenyeviti wa serikali za vijiji kunyanyasa wafanyakazi, wakiwamo walimu jimboni mwake bila kuchukua hatua.

"Wafanyakazi wakiomba kuhama kutoka Musoma Vijijini tutawalaumu? Je, tunapolalamika kuhusu upungufu mkubwa wa wafanyakazi, tunajua tulisemalo?," Profesa Muhongo alihoji wakati akizungumzia tukio hilo.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mara, Salim Morcase, alipotafutwa alisema tukio hilo bado halijafika ofisi kwake, mpaka afuatilie.

# SUA yajitosa utafiti maji

**Na Ashton Balaigwa**

CHUO Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kilichopo mkoani Morogoro, kinafanya utafiti wa kubaini tatizo la ukosefu wa maji katika maeneo yenye ukame ili kupata suluhisho la kutatua changamoto hiyo inayoikabili baadhi ya mikoa.

Utafiti huo unafanyika kupitia Mradi wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi na Ustahimilivu katika Nyanda Kavu za Kitropiki (CLARITY).

Mtafiti Mkuu wa Mradi huo, Prof. Japhet Kashaigili, alisema wanaanza utafiti jijini Dodoma ambalo ni moja ya mikoa inayokabiliwa na tatizo la maji kutokana na ukame.

Katika mkutano wa kutambulisha mradi huo uliofanyika jijini Dodoma, Prof. Kashaigili alisema lengo ni kuboresha na kuongeza kasi ya upatikanaji wa maji mkoani humo. Alisema mradi huo unaotekelezwa kwa miaka mitatu na nusu, matokeo ya utafiti yatasaidia kuelewa namna mabadiliko ya tabianchi yatavyoathiri upatikanaji wa maji, matarajio au hatua za kuchukua kwa maendeleo ya baadaye.

Prof. Kashaigili alisema umelenga kubaini changamoto na kupata suluhisho bunifu kupitia utafiti wa kitaalamu katika fani tofauti.

Mtafiti Msaidizi wa Mradi huo, Dk. Devota Mosha alisema anaamini utatoa suluhisho endelevu la changamoto ya maji jijini Dodoma.

Alisema mradi huo unafadhiliwa na Kituo cha Utafiti wa Maendeleo ya Kimataifa (IDRC Canada), serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Jumuiya ya Madola na Maendeleo (FCDO, Uingereza) chini ya mpango wa Kukabiliana na Hali ya Hewa na Ustahimilivu (CLARE).

Katibu Mkuu Wizara ya Maji, Prof. Jamal Katundu, alisema wanaamini matokeo ya utafiti huo yatasaidia kutatua changamoto zitokanazo na mabadiliko ya tabianchi pamoja na za upatikanaji wa maji mkoani Dodoma.

Alisema SUA imefanya jambo jema kuichagua Dodoma kwa kuwa ni moja ya mikoa inayokabiliwa na hali ya ukame, hivyo matokeo ya utafiti yatasaidia mikoa mingine yenye tatizo kama hilo.

Alisema takwimu zilizopo, Tanzania ina hali nzuri ya upatikanaji wa rasilimali maji zipatazo mita za ujazo bilioni 126 kwa mwaka, ambapo mita za ujazo bilioni 105 ni maji juu ya ardhi na ujazo wa bilioni 21 ni maji chini ya ardhi.

"Kwa takwimu hizo tafsiri yake ni kuwa, katika ardhi kame kama Dodoma wakati mnafanya utafiti itaweza kutusaidia kuja na suluhisho la kutatua changamoto ya maji katika maeneo yaliyo na ukame," alisema Prof. Katundu.

Mkurugenzi wa Utafiti na Uzamili, Prof. Ezron Karimuribo, akizungumza kwa niaba ya Makamu Mkuu wa SUA, Prof. Raphael Chibunda, alisema chuo hicho kimekuwa kikifanya utafiti mbalimbali kwa kushirikiana na wadau wa ndani na nje ya nchi ili kuongeza nguvu katika kupata majawabu ya changamoto mbalimbali. "Sisi sio kisiwa ni sehemu ya dunia, kwa hiyo tunafanya hivi tukijua wazi kwamba mabadiliko ya tabianchi yakitokea sehemu yoyote yanaweza kuleta madhara nchini. "Ni wajibu wetu kufanya utafiti na ugunduzi wa teknolojia mbalimbali ili ziweze kusaidia katika kutatua changamoto mbalimbali," alisema.

# Shahidi afichua taarifa gari linalodaiwa kutumika mauaji dada Bilionea Msuya

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Dar es Salaam, imeelezwa kwamba gari linalodaiwa kutumiwa na aliyekuwa mke wa Bilionea Msuya, Marehemu Erasto Msuya, Miriam Mrita, kwenda nyumbani kwa wifi yake, Aneth Msuya, Mei 15, 2016 kabla ya kuuawa. Kwa tarehe hiyo lilikuwa gereji.

Aidha, imeelezwa gari hilo ni lenye namba za usajili T 307 CDH aina ya Ford Ranger lilikuwa kwenye kampuni ya kuuza magari ya CMC Automobiles Ltd kwa ajili ya matengenezo kutokana na kwamba lilikuwa bovu.

Hayo yalidaiwa jana na Meneja Utawala na Matengenezo kutoka Makao Makuu ya kampuni hiyo jijini Dar es Salaam, Ernest Msuya, mbele ya Jaji Edwin Kakolaki wakati akitoa ushahidi wa kumtetea Mrita anayetuhumiwa kumuua wifi yake huyo.

Katika utetezi wake, alidai kuwa tarehe ambayo aliambiwa alikwenda nyumbani kwa wifi yake Kibada, Kigamboni kabla ya mauaji kutokea, gari hilo lilikuwa gereji kutokana na ajali ambayo ilikuwa imetokea wakati anarudi kutoka Nairobi kupeleka watoto shule. Akiongozwa na Wakili Peter Kibatala, alidai kuwa gari hiyo tangu liuzwe na kampuni hiyo mwaka 2012 wao ndio walikuwa wanalifanyia matengenezo kwa sababu bado lilikuwa ndani ya waranti. Alidai kuwa gari hilo liliuzwa katika tawi lao lililokuwapo Arusha na kwamba matawi yao yote yanafuata maelekezo kutoka makao makuu ndiyo maana yeye ana taarifa zote kuhusiana na gari hilo licha ya kwamba yuko Dar es Salaam.

Shahidi huyo, baada ya kupewa nyaraka (mwenendo wa gari) na Wakili Kibatala, aliitambua kuwa inatoka ofisini kwao Arusha ambayo ilitumwa jana na ikafika katika ofisi yao ya Dar es Salaam na kisha wakili akaichukua. "Mheshimiwa Jaji naomba mahakama ipokee nyaraka ya mwenendo wa gari namba T 307 CDH aina ya Ford Ranger tangu mwaka 2012 kama kielelezo. Ina taarifa za lini gari liliingia kwa matengenezo na kutoka," alidai na kuomba.

Mahakama hiyo ilipokea kielelezo hicho na kuwa DE 11 kutokana na upande wa mashitaka ukiongozwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Paul Kimweri, kutokuwa na pingamizi.

Baada ya nyaraka hiyo kupokelewa, shahidi aliruhusiwa na mahakama kuisoma na kudai kuwa gari hilo lilirudi kwa matengezo katika kampuni yao kwa zaidi ya mara 10 na lilikuwa na tatizo la kugonga kwa injini.

Akifafanua baadhi ya tarehe, alidai kuwa Mei 15, 2016, Mei 18, 2016, Mei 20, 2016, Mei 23, 2016, Mei 25,2016 na Mei 26, 2016 gari hilo lilikuwa gereji katika kampuni hiyo kwa sababu lilikuwa bovu limerudishwa kwa matengezo.

Akiendelea kutoa ufafanuzi, Ernest alidai kuwa Agosti 10, 2016 gari hilo liliingia na kilometa 30,569 na lilitoka likiwa na kilometa 30,573, kwa hiyo lilizunguka kwa kilometa nne tun a hadi sasa bado liko CMC kwa sababu haliwezi kutembea.

"Walikuja askari polisi kutoka Arusha, wakataka kuchukua gari hili lakini wakaelezwa kwamba ni bovu na halina uwezo wa kutembea umbali mrefu. Polisi walilazimisha wakalichukua, hawakufika nalo mbali wakalirudisha,. "Na kwa kitendo hicho walichokifanya mteja alikuwa hana taarifa wakati polisi wipokuja yaani kama yupo hapa basi ndiyo anayasikia haya kwa sababu ilikuwa ni kati yetu sisi na polisi," alidai Ernest.

Pia alidai kuwa kwa ubovu wa gari hilo, Mei 15,2016 hakukuwa na uwezekano wowote wa kutoka kutokana na ubovu lililokuwa nayo. Kwa kipindi chote hicho dereva ambae alikuwa akilipeleka gari hilo ni Karim Mruma.

Kwa upande wa mashitaka wanamtuhumu Mrita jkwamba Mei 15, 2016 alitumia gari namba T 307 CDH aina ya Ford Ranger kwa mara ya kwanza kwenda nyumbani kwa wifi yake, Aneth Msuya, kabla ya kabla ya kuuwawa Mei 25, 2016.

Kesi hiyo imeahirishwa hadi Jumatatu, ambapo jopo la mawakili wa Serikali litamuuliiza maswali dodoso shahidi Ernest kutokana na alichokizungumza mahakamani. Miriam ambaye ni mshtakiwa wa kwanza katika kesi ya mauaji ya wifi yake, Aneth, aliyeuawa Mei 25, 2016 kwa kuchinjwa nyumbani kwake, Kibada Kigamboni mkoani Dar es Salaam. Alikiri kuhusika na mauaji hayo katika maelezo yake ya onyo. Mshitakiwa wa pili katika kesi hiyo ni Revocatus Muyela.

# Mpango wa uchumi wa buluu wafungua milango ya ajira

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Uvuvi wa Bahari Kuu, imesema mpango wa uchumi wa buluu umefungua mlango wa ajira tangu kuanza utekelezaji wake baada ya kuanzishwa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka hiyo, Dk. Emanuel Andrew Sweke, aliyasema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari, kuhusu utekelezaji wa mpango huo katika kipindi cha miaka mitatu tangu Rais Mwinyi kushika wadhifa huo.

Alisema kasi ya usajili wa meli ya uvuvi wa Bahari Kuu imekuwa ikiongezeka baada ya mamlaka hiyo kutoa leseni 100 za uvuvi wa bahari kuu zikiwamo kampuni za kimataifa.

“Kuna ajira za moja kwa moja ambazo zimesaidia kufikia lengo la serikali katika utekelezaji wa ilani ya uchaguzi, kutoa ajira 300,000 kwa wananchi wa Zanzibar katika kipindi cha miaka mitatu cha serikali ya awamu ya nane,” alisema Dk. Sweke.

Alisema mpaka sasa mabaharia 14 kutoka Zanzibar na Tanzania Bara wameajiriwa katika meli za uvuvi wa bahari kuu na tayari wawekezaji kutoka nje na ndani ya nchi wameanza kujitokeza kuwekeza katika sekta hiyo.

Dk. Sweke alisema mchakato wa kuanzishwa kiwanda cha kuchakata minofu ya samaki umeanza kufanyika kikilenga kutoa ajira zaidi ya watu 100, mbali na wachuuzi ambao watanufaika na samaki watakaotayarishwa na kiwanda hicho.

“Katika mwaka wa fedha 2019/2020, hatukuweza kutoa leseni hata moja za uvuvi wa bahari kuu kutokana na mazingira yaliokuwa yamejitokeza yakiwamo maradhi ya UVIKO-19, lakini kuanzia mwaka 2020 hadi 2023 tumetoa leseni 100 kutoka leseni 30 zikiwamo kampuni za uvuvi za kimataifa,”alisema Dk. Sweke.

Alisema tokea kuanzishwa kwa mamlaka hiyo mwaka 2010, sekta ya uvuvi imeanza kuchangia kiwango kikubwa pato la taifa hasa baada ya kuanzishwa mpango wa uchumi wa buluu wa kuongeza uzalishaji kupitia maliasili za baharini.

Alisema kwa mujibu wa sheria ya mamlaka hiyo, serikali ya Jamhuri ya Muungano imekuwa ikinufaika na asilimia 30 ya mapato, asilimia 20 serikali ya Zanzibar na asilimia 50 hunufaika mamlaka ya uvuvi wa bahari kuu Tanzania. Dk. Sweke alisema kwamba mamlaka hiyo mpaka sasa inaendelea na majukumu yake ambayo mbali na kutoa leseni za uvuvi wa bahari kuu, pia kuhakikisha meli za uvuvi zinazingatia suala la uhifadhi wa mazingira ya bahari kwa usalama wa rasilimali zake.

Akizungumza kuhusu mafanikio yaliopatikana chini ya mpango wa uchumi wa buluu, Katibu mkuu wa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi, Dk. Aboud Suleiman Jumbe, alisema umefungua mlango mpya wa kuchagia pato la taifa kwa Zanzibar .

“Sekta ya uvuvi imeonesha mwelekeo mzuri katika kuchagia pato la taifa kwa asilimia 6.32 kutoka asilimia 4.5 kuanzia mwaka 2020 hadi mwaka 2022,” alisema.

Dk. Jumbe alisema wakati serikali ya awamu ya nane inaingia madarakani uzalishaji wa samaki ulikuwa tani 38,107 zenye thamani ya Sh. bilioni 205.4 kwa mwaka na sasa umefikia tani 61,794 zenye thamani ya Sh. bilioni 391.37 kwa mwaka.

Alisema miradi ya sekta ya uvuvi imeongezeka kutoka mradi mmoja hadi 17 yenye thamani ya Sh. bilioni 337.5, kutoka Sh. bilioni 10, huku wavuvi wadogo wakifaidika na boti za kisasa 577 ambazo zitawezesha kuvua katika kina kirefu na kuongeza kipato.

Rais Mwinyi anatimiza miaka mitatu huku mwelekeo wa serikali yake ukiweka kipaumbele katika ujenzi wa miradi ya barabara, kuimarisha huduma za afya, elimu pamoja na kuwajengea uwezo wavuvi wadogo na kuwapatia mikopo wajasiriamali visiwani humo.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Mtumba,
S.L.P. 2888,
40470DODOMA,
04.11.2023

## TAARIFA KWA UMMA

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta Ujenzi) inapenda kuutaarifu umma kuwa siku ya Jumanne tarehe 17-10-2023 hadi 20-10-2023 kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** itasafirisha Mzigo wenye vipimo vikubwa kutoka **Dar-Es-Salaam Port** kuelekea **Rufiji,** gari ilo lina namba ya usajili

**T 116 EDS / T 630 AJA**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
   **Urefu - mita 24.00**
   **Upana - mita 4.40**
   **Kimo - mita 4.60**

3. Njia itakayotumika: Dar-Es-Salaam, Pwani hadi Rufiji kupitia Kibiti, gari zitasafiri muda wa mchana tu (Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza**


# Asasi yasisitiza upatikanaji wa haki kujenga jamii imara

**Na Romana Mallya**

MKURUGENZI Mtendaji wa Legal Services Facility (LSF), Lulu Ng’wanakilala, amesema upatikanaji wa haki ni muhimu katika kujenga jamii zenye amani, haki na imara.

Amesema dhamira yao imejikita katika kanuni ya kuendeleza hayo ili kuchangia kwa kiasi kikubwa katika kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs).

Akizungumza juzi jijini Dar es Salaam, Lulu alisema mwaka 2022, LSF ilifikia moja kwa moja zaidi ya wanajamii milioni 6.4 kutoka Bara na Visiwani Zanzibar, na kwa njia isiyo ya moja kwa moja iliwafikia watu milioni 10 kupitia vyombo vya habari.

Alisema kwa mwaka wamekuwa wakifikia watu milioni saba kupitia elimu ya kisheria na hupokea migogoro 70,000 ambapo asilimia 60 hutatuliwa na wasaidizi wa kisheria, hivyo kupunguza msongamano mahakamani.

Lulu alisema wameweza kutoa misaada mikubwa yenye thamani ya Sh. bilioni 4.7 kusaidia waathirika wa Unyanyasaji wa Kijinsia (GBV) na kushirikiana kikamilifu na Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia.

Vilevile alisema wanashirikiana na serikali na Mashirika ya Kiraia (CSO), kupanua msaada muhimu kwa waathirika wa GBV.

Alisema LSF imejipanga kwa dhati kuinua ustawi wa kiuchumi wa wanawake na kuboresha matarajio ya familia ikiwiana na Mpango Mkakati wa Umoja wa Mataifa wa Wanawake wa 2022-2025.

“Mpango huu unatambua kuwa kuwekeza katika uwezeshaji wa wanawake kiuchumi kunafungua njia ya usawa wa kijinsia, kutokomeza umaskini na ukuaji wa uchumi jumuishi,” alibainisha Mkurugenzi huyo.

Lulu alisema LSF inaamini kuwa upatikanaji wa haki ni muhimu kwa ajili ya kujenga jamii zenye amani, haki na imara.

“Kazi yetu imejikita sana katika kuendeleza kanuni hizi, na hivyo kuchangia kwa kiasi kikubwa SDGs. Lengo namba 16 la SDGs za Umoja wa Mataifa, kuhusu ‘Amani, Haki, na Taasisi Imara’ ni kiini cha safari ya Tanzania ya kufikia maendeleo endelevu,” alisema.

Hata hivyo, Mkurugenzi huyo alisema mpango wa LSF wa kupata haki unakabiliana na vikwazo vya kitamaduni na unatoa huduma muhimu za msaada wa kisheria kwa walio hatarini zaidi hususani wanawake, wasichana na jamii zilizotengwa.

Lulu alisema LSF inafanya kazi kwa kanuni kwamba watu walio na ufahamu mzuri na thabiti wa haki zao na mfumo wa kisheria, wana nyenzo mahiri zaidi kwa uwezeshaji wa kijamii na kiuchumi.

Alisema LSF imesuluhisha migogoro 3,176 ya mirathi, huku 1,172 ikipendelea wanawake, ikiimarisha jukumu lao katika kupata ufikiaji wa kundi hilo kwa mali muhimu ambacho ni kipengele cha SDG 5 (usawa wa kijinsia).

Alisema wanasimama kama mtetezi aliyejitolea wa usawa wa kijinsia na uwezeshaji wa wanawake ambapo mwaka 2022, waliwafikia wanawake na wasichana.



## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Simba, Yanga mashabiki wahitaji ubora, burudani

**MASHABIKI** mbalimbali wa soka wa ndani na nje ya Tanzania wanatarajia kushuhudia mechi ya watani wa jadi, Simba na Yanga itakayochezwa kesho kuanzia saa 11:00 jioni kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Mechi hiyo ni ya mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo inaingia katika raundi ya tisa, lakini Simba ikiwa na kiporo cha mchezo mmoja, kilichotokana na ushiriki wake wa mashindano ya kimataifa ya African Football League (AFL).

Hata hivyo, hiyo itakuwa ni mechi ya pili kwa vigogo hao kukutana, mchezo wa kwanza walikutana katika fainali ya Ngao ya Jamii iliyochezwa Agosti 13, mwaka huu kwenye Uwanja wa CCM Mkwakwaji jijini, Tanga. Simba alishinda fainali hiyo na kuanza msimu mpya kwa taji.

Hata hivyo timu hizo zinakutana pia msimu huu kila moja ikiwa imetinga hatua ya makundi ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, hivyo mbali na kupambana kusaka ushindi, zitakuwa zinatumia mchezo huo kuendelea na maandalizi yake kuelekea hatua hiyo muhimu.

Ni wazi kila timu itashuka uwanjani ikiwa na malengo ya kusaka ushindi na ikishindikana kugawana pointi lakini si kuamini itapoteza mechi hiyo ya dabi ambayo huwa na 'joto la mapambano' ndani na nje ya uwanja.

Makocha wote wamekuwa na muda wa kurekebisha mapungufu lakini kuimarisha zile idara zinazofanya vizuri, pamoja na kuwasoma wapinzani, haya yote yanafanyika kwa sababu ya kusaka ushindi na kuweka heshima, hivyo ni mechi ambayo itakuwa na ushindani zaidi kutokana na mafanikio yaliyoko ya kila upande.

Wakati makocha wanaumiza kichwa kuandaa mbinu zitakazowapa ushindi, wachezaji wanatakiwa kufahamu mechi hii ni daraja la juu kwao kujiuza kwa sababu wapinzani wao katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika watakuwa wanawafuatilia.

Kwanza wafahamu watafuatiliwa ili kujua mbinu zao na kujipanga kuwakabili watakapokutana, lakini pia kuwasajili kwa wale ambao watakaoonyesha viwango bora katika mchezo huo.

Tunawakumbusha mbali na kuonyesha viwango vya juu, wachezaji wanatakiwa kucheza kwa nidhamu, mchezaji mwenye nidhamu nzuri anajiongezea thamani na kwa kufanya hivyo, mechi hiyo inaweza kufungua ukurasa mpya wa maisha ya baadhi ya nyota ambao wanahitaji kuzitimiza ndoto zao kwa kwenda kusakata kandanda la kulipwa katika mataifa ya Ulaya.


Jambo lingine muhimu ni kuwakumbusha waamuzi watakaopewa dhamana ya kusimamia mechi hiyo kufuata sheria 17 za mchezo huu, kuongeza umakini na utulivu katika kila tukio, kwa kifupi wanasema kuchezesha kwa haki ili timu itakayostahili kupata ushindi, ipate ushindi huo na isionekane imevuna pointi kwa kubebwa.

Mashabiki wanatakiwa wafahamu mechi hiyo itarushwa mubashara na hivyo dunia itakuwa inaangalia yote yanayoendelea ndani na nje ya uwanja, utulivu na nidhamu yao ni mtaji mkubwa kwa Tanzania na Shirikisho la Soka Nchini (TFF), kuendelea kuaminiwa kuandaa mashindano mbalimbali ya kimataifa kama ambavyo tulivyoshuhudia kufana kwa ufunguzi wa michuano ya African Football League (AFL).

Nipashe pia inawakumbusha viongozi, wachezaji, wanachama na mashabiki wa timu zote mbili kuwa na kauli za kiungwana kabla na baada ya matokeo, haipendezi kusikia kauli ambazo haina faida na afya katika maendeleo ya soka letu baada ya kumalizika kwa dabi hiyo, na hasa kauli hizo hutolewa na timu iliyopoteza.

Tukumbuke mechi ya mpira wa miguu ina matokeo ya aina tatu, hivyo kila upande unatakiwa kukubaliana na matokeo ambayo timu yake itayapata, mpira ni furaha, mpira ni ajira.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

### Dabi inahitaji ufundi, mvuto ubabe umepitwa na wakati

**AFRIKA** Mashariki na Kati pamoja na nchi mbalimbali Afrika kesho kuanzia saa 11:00 jioni zitasimama kwa dakika 90 kupisha mechi ya watani wa jadi, wakati Simba itakapoikaribisha Yanga kwenye Uwanja wa Banjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Nasema hivyo kwa sababu mechi za Dabi ya Simba na Yanga kwa sasa zimevuka mipaka na kuvutia mashabiki wengi wa soka wa sehemu mbalimbali ndani na nje ya Afrika.

Zamani ni Tanzania ilikuwa na homa hiyo, ambapo dakika 90 zilikuwa zikisimama kupisha mechi hiyo, lakini kwa sasa dabi ya Bongo imepiga hatua kubwa kiasi imekuwa mfano wa kuigwa kwa nchi nyingi, lakini pia zilipoanza kuchukua wachezaji wa kigeni kutoka mataifa mengine, mashabiki wa nchi hizo nao wameonekana kuzifuatilia ili kuangalia wachezaji wao.

Ndiyo maana usishange kuona dabi hiyo ikileta msisimko na kufuatiliwa na mashabiki si Tanzania, Kenya, Uganda, bali hata Zambia, Mali, Senegal, Sudan, Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC), Cameroon, Ghana, Rwanda, Burundi, Mali na nyinginezo.

Ni jambo la kushukuru tangu miaka ya 1940 wakati timu hizo bado changa hadi leo, zimekuwa na umaarufu mkubwa kila miaka inavyozidi kwenda zimeonekana kujiongezea mashabiki, dabi yao ikiendelea kuwa na mvuto kwa sababu baadhi ya nchi kama Kenya, Uganda na zingine chache, msisimko wa dabi zao umekuwa wa chini mno.

Inawezekana kabisa ukiondoa mvuto wa mechi za Al Ahly na Zamalek, dabi ya Afrika Kusini kati ya Orlando Pirates na Kaizer Chiefs na Wydad Casablanca na Raja Casablanca za Morocco, dabi hii ya Kariakoo inafuatia kwa msisimko, mvuto, na kufuatiwa na mashabiki wengi.

Kwa maana hiyo, napenda kuwasihi wachezaji wa pande zote mbili wanapoingia uwanjani, waache kila kitu nje, wapambane kwa hali na mali, wavuje jasho, watoke machozi na kutoka damu kwa ajili ya nembo za klabu zao.

Wachezaji wanatakiwa waonyeshe vipaji vyao ambavyo vimewafanya kufika hapo walipo na si kucheza kwa kupaniana, rafu za kishamba, fujo au kukoromeana na kutisha waamuzi.

Soka la sasa limeshatoka huko, wachezaji wanatakiwa kujua kila kitu cha kihuni wanachokifanya kinatazamwa kwenye televisheni, hata kama mwamuzi hakuona na kuchukuliwa hatua, lakini watahukumiwa na mashabiki wa soka pamoja na mawakala ambayo wanatizama kupitia mitandao ya kijamii.

Kwa upande wa waamuzi watakaopewa dhamana ya kuchezesha mechi hiyo, nao wanatakiwa wawe kama mahakimu wa mahakamani, wanatakiwa kutenda haki kiasi isiwape mada mashabiki wa wachambuzi kuona kuna umuhimu sasa wa kushusha waamuzi kutoka nje ya nchi ili kuja kuchezesha 'dabi.'

Wachezaji wengi kwa sasa wamekuwa wakitumia udhaifu na uoga wa waamuzi kucheza rafu mbaya kwa wenzao na wamekuwa hawaonywi, mpaka zifika tano hadi sita, ndipo kadi ya njano zitoke.

Waamuzi wanatakiwa kuwalinda wachezaji wanaotaka kucheza soka na kuburudisha mashabiki dhidi ya wacheza rafu, waamuzi hawatakiwa kusawazisha makosa, yoyote anayefanya kosa lolote lile adhabu itoke hapo hapo.

Hiyo itawafanya wasiwe na wasiwasi au 'kubalansi' mchezo. Kuachia au kupeta makosa fulani uwanjani inamwondoa mchezoni kwani anashinda kuamua kosa lingine likifanywa na mwingine kwa sababu ya kusawazisha makosa.

Mashabiki wanataka Jumatatu wakiamka majina yanayotajwa yawe ya wachezaji jinsi walivyotakata na si mada ni idadi ya makosa ya waamuzi.

Hivi karibuni kumekuwa na video fupi ikizunguka kwenye mitandao ya kijamii ikionyesha mashabiki wanaodhaniwa ni wa Simba wakimpiga wa Yanga.

Hii isijirudie tena, si kwenye mechi ya kesho bali zote zinazofuata. Soka ni upendo, amani, kufahamiana na kudumisha umoja.

Kinachotakiwa mechi ikiisha watu waondoke salama, asikanyagwe hata sisimizi.

Na huo ndiyo utamaduni wa Watanzania na tumeonyesha kwenye mechi za hivi karibuni za Ligi ya Mabingwa Afrika, Kombe la Shirikisho na hata katika ufunguzi wa michuano ya African Football League (AFL). Nawatakia mchezo mwema.

# TANROADS kutia saini mikataba ya tril. 1.034/- kuboresha miundombinu

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI kupitia Wakala ya Barabara Tanzania (TANROADS) inatarajia kutia saini mikataba 15 kwa pamoja ya ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami pamoja na daraja zenye thamani ya Sh. trilioni 1.034 ili kuboresha huduma za miundombinu nchini.

Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashungwa, aliyasema hayo jana wakati akitoa majibu ya nyongeza bungeni jijini Dodoma katika kikao cha Nne, Mkutano wa 13.

Bashungwa alisema kuwa miradi hiyo inatarajiwa kutekelezwa kwa kutumia fedha za ndani za miradi ya maendeleo na Serikali iko mbioni kuandaa tukio hilo.

"Mheshimiwa Rais (Samia Suluhu Hassan) ameshatoa kibali kama mheshimiwa Naibu Waziri alivyosema na tumeona tuandae siku ambayo tutasaini mikataba hii kwa siku moja halafu baada ya hapo mimi na Naibu Waziri tutaambatana na Waheshimiwa Wabunge kwenda kuwakabidhi makandarasi kwenye majimbo yenu," alisema Bashungwa.

Naibu Waziri wa Ujenzi, Mhandisi Godfrey Kasekenya wakati akijibu swali la Mbunge wa Busokelo, Atupele Mwakibete, alisema taratibu za ununuzi wa mkandarasi kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami kwa sehemu ya barabara ya Katumba - Lupaso (km 35.3) na Kibanja - Tukuyu (km 20.7) zimekamilika, hatua inayofuata ni kumkabidhi mkandarasi eneo la kazi.

Kasekenya alikuwa akijibu swali la Atupele Mwakibete, Mbunge wa Busokelo aliyetaka kujua ni lini lini mkataba wa ujenzi wa barabara ya Katumba - Mbambo hadi Tukuyu utatiwa saini kwa kuwa mkandarasi alishapatikana.



Daktari Bingwa wa Magonjwa ya wanawake, uzazi na upasuaji wa fistula kutoka hospitali ya CCBRT, Peter Majinge akifurahia jambo na mmoja wa wagonjwa wake wa fistula, wodini hospitali ya Mkoa wa Lindi-Sokoine jana, baada ya kukamilika kwa matibabu yake wakati wa kambi ya wiki moja ya matibabu ya ugonjwa wa fistula iliyomalizika hospitalini hapo. Tangu mwaka 2019 CCBRT, Equinor Tanzania na mkoa wa Lindi wamekuwa katika ubia wa kutoa matibabu ya ugonjwa huo kwa wanawake mkoani Lindi, sambamba na kuwawezesha kiuchumi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

# Waziri ataka utatuzi changamoto TANESCO

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri wa Nishati, Judith Kapinga, ameutaka uongozi wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kutatua changamoto sugu zinazokabili wananchi kwa kufanya kazi za ziada ili kupata mabadiliko katika utoaji wa huduma.

Judith aliyasema hayo juzi jijini Dodoma alipokutana na uongozi wa TANESCO kwa lengo la kuzungumza nao na kufahamu namna walivyojipanga katika kutatua changamoto mbalimbali za umeme kwa wananchi.

Kiongozi huyo amelitaka shirika hilo kuweka mipango ya muda mrefu ili kumaliza changamoto ndogondogo akitolea mfano tatizo la kukatika kwa umeme na kero zinazowakabili wananchi.

"Dunia imeendelea sana na teknolojia imekuwa mno, umeme kwa sasa si anasa, hivyo kila mtu anahitaji huduma hiyo kwa matumizi ya aina mbalimbali, tuhakikishe tunawafikia wananchi ili waendane kulingana na dunia ya sasa," alisisitiza Kapinga.

Pia alilitaka shirika hilo kuongeza kasi ya kuunganisha wateja wapya kwa kuwafikishia huduma ya umeme maeneo ambayo bado hayajafikiwa.

Kadhalika, ameutaka uongozi huo kuwashirikisha na kuwafahamisha viongozi wa chama na serikali wakiwamo wakuu wa mikoa, wakuu wa wilaya na watendaji wa Serikali za Mitaa kuhusu miradi mbalimbali inayoendelea katika maeneo yao, ili wafahamu vema na kuwaeleza wananchi wanaowaongoza.

Kadhalika amelitaka shirika hilo kusimamia kwa ukaribu miradi ya vipaumbele ukiwamo wa kupeleka umeme Katavi, Rukwa, Kigoma, Kagera, Mtwara na Lindi. Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO, Mhandisi Gissima Nyamohanga, amemweleza Naibu Waziri kuwa wamepokea maelekezo hayo na wapo tayari kwa utekelezaji.

Mkutano huo pia, umehudhuriwa na Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Athumani Mbuttuka, Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Innocent Luoga na viongozi wengine waandamizi kutoka TANESCO.

# Tanzania yapendekeza AGOA iongezwe miaka 20

**Na Joseph Mwendapole**

TANZANIA imependekeza Mpango wa Ukuaji na Fursa wa Afrika (AGOA) uongezewe kipindi kingine cha miaka 20, awamu ya kwanza itakapofika ukomo wake mwaka 2025.

Ombi hilo lilitolewa jana na Waziri wa Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji, wakati akichangia mjadala kuhusu utekelezaji wa AGOA unaoendelea Johannesburg nchini Afrika Kusini katika kongamano la 20 linalofanyika kwa siku nne.

Dk. Kijaji alisema kuongezwa kwa kipindi kirefu zaidi kutasaidia utekelezaji wa AGOA na kuchochea uwekezaji wa muda mrefu katika nchi za Afrika kuliko kipindi cha maka 10 ambacho hakiwezi kutoa matokeo chanya na makubwa kwa wawekezaji.

Pia alisisitiza haja ya kuruhusu AGOA iweze kujumuisha nchi zote wanachama wa Makataba wa Eneo Huru la Biashara Afrika (AfCFTA ) na kuimarisha ushirikiano kati ya AGOA na AfCFTA.

Aidha, alisema kujumuishwa kwa nchi hizo kutasaidia kuunga mkono juhudi za ushirikiano wa kikanda ili kupanua wigo wa AGOA pamoja na kuzingatia masuala mengine muhimu kama vile biashara ya huduma.

Kuhusu vigezo vya kuingia AGOA, Dk. Kijaji alisema nchi ambazo zimefikia hadhi ya kipato cha juu hazipaswi kutolewa mara moja kutoka kwa programu ya AGOA, kwani nchi nyingi zinaendelea kupata shida za kiuchumi na ukosefu wa ajira.

Pia aliomba marekebisho ya ukaguzi wa vigezo au sifa za kujiunga AGOA kufanyika kila baada ya miaka mitatu badala ya ukaguzi wa kila mwaka kama ilivyo sasa. "Kuongezwa kwa muda kutajenga ujasiri na muda zaidi kwa wawekezaji kufanya tathmini na kuchukua hatua za kurekebisha panapohitajika na naipongeza Marekani na Serikali ya Afrika Kusini kwa maandalizi mazuri ya mkutano wa mwaka huu," alisema.

Alisema Tanzania itaendelea kuipongeza Marekani kwa kuanzisha program ya AGOA, ambao umekuwa na manufaa makubwa kwa wafanyabiashara wa hapa nchini. "Lakini hata hivyo bado wafanyabiashara wetu hawajatumia hii fursa vizuri nashukuru kwamba waandaaji wa mkutano wameweka mikutano midogo midogo ya kujadili jambo hili kwa hiyo naamini tutapata muda wa kulijadili," alisema.




Mwanafunzi wa darasa la sita katika Shule ya Msingi Kibugumo, Feisali Msiakwe akinyanyua juu kikombe chake baada ya kuibuka mshindi wa mchoro wa kuelimisha usalama barabarani katika shindano lililoandaliwa na Kampuni ya Mafuta ya Puma Tanzania kwa kushirikiana na Shirika la Amend, jijini Dar es Salaam juzi. Feisali amejipatia kitita cha 500, 000/- na kuifanya shule yake kupata Sh. milioni 5. Kushoto ni Mkurugenzi Mtendaji wa Puma Tanzania, Fatma Abdallah. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wataalam wa madini wanolewa Indonesia

**Na Mwandishi Wetu**

WATAALAM wapatao 20 kutoka Wizara ya Madini na taasisi zake wameanza rasmi mafunzo ya kujengewa uwezo wa masuala mbalimbali ikiwamo utafiti, usalama wa makaa ya mawe pamoja na madini mengine katika Kituo cha Human Resource Development Center Geology, Minerals nchini Indonesia.

Mafunzo hayo yanafanyika ikiwa imepita takribani kipindi cha miezi sita baada ya kufanyika mazungumzo na makubaliano ya ushirikiano katika nyanja mbalimbali katika sekta ya madini ikiwamo kuwaendeleza watumishi na wataalam.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na wizara hiyo, lengo la mafunzo hayo ni kuwajengea uwezo katika kusimamia na kuendeleza rasilimali madini.

Taarifa hiyo ilisema mwezi Mei, mwaka huu, Tanzania kupitia aliyekuwa Waziri wa Madini ambaye kwa sasa ni Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko na Balozi wa Indonesia nchini Tanzania, Tri Yogo Jatmiko walijadili kuhusu kuwekeza katika shughuli za uchimbaji.

Pia ilisema walijadili suala la ushirikiano kupitia Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) na Taasisi ya uchimbaji wa madini ya nchini Indonesia inayoitwa Mining Industry Indonesia. Kadhalika, ilisema masuala mengine yaliyojadiliwa katika kikao hicho yalikuwa ni pamoja na fursa za mafunzo ya shughuli za uchimbaji nchini humo ikiwemo usalama migodini.

"Katika siku za awali za mafunzo hayo, ilielezwa kuwa ushirikiano kati ya Tanzania na Indonesia umekuwapo tangu mwaka 1955 ambapo serikali ya Indonesia ilishiriki katika ukombozi wa Nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara.

"Hatimaye nchi ilijenga ubalozi wake jijini Dar es Salaam mwaka 1964 na Tanzania ilianzisha ubalozi wake mwaka 2022 katika jiji la Jarkata nchini humo," ilieleza taarifa.

Pia ilisema kama ilivyobainishwa katika vipaumbele vya wizara kwa mwaka wa fedha 2023/24, miongoni mwake ni kuendeleza madini muhimu na mkakati na kuzijengea uwezo taasisi zake ziweze kutekeleza majukumu yake. Ilisema kuwa kufanyika kwa mafunzo hayo kunadhihirisha dhamira ya wizara kufikia malengo yaliyopangwa.

Ilisema matokeo yanayotarajiwa ni kuwawezesha maofisa wa wizara na taasisi zake kuwa na ujuzi stahiki wa kuchambua, kusimamia na kukagua miradi ya uwekezaji katika sekta na kushauri namna bora ya kiwezesha miradi hiyo kupata mitaji ya kuwekeza ipasavyo.

# Mradi wa bil. 40/- kumaliza kero ya maji kwa wakazi 450,000 Dar

**Na Joseph Mwendapole**

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira (DAWASA), imetia saini mkataba na kampuni ya Sinohydro Corporation Ltd wa ujenzi wa mradi wa maji utakaogharimu Sh. bilioni 40 ambao utanufaisha wananchi 450,000 baada ya kukamilika.

Wananchi wa majimbo ya Kibamba, Segerea, Ukonga, Ubungo,Temeke na Ilala wanatarajiwa kunufaika baada ya kukamilika kwa mradi huo utakaotekelezwa kwa miaka miwili.

Hafla ya kutiliana saini ilifanyika juzi kwenye ofisi za DAWASA baina ya Mkurugenzi wa Sheria wa Mamkaka hiyo, Florence Yamatim na mwakilishi wa Sinohydro Corporation Ltd na kushuhudiwa na Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu wa DAWASA, Kiula Kingu.

Akizungumza kwenye hafla hiyo, Kingu alisema mkataba huo unahusu ujenzi wa miundombinu ya usambazaji maji Dar es salaam ya Kusini ambao utahusisha ujenzi wa tanki kubwa la kuhifadhi maji la lita milioni tisa.

Alisema mkataba huo utahusu pia ujenzi wa kituo cha kusukuma maji na ulazaji wa bomba kwa umbali wa kilomita 25 na unatarajiwa kunufaisha wananchi 450,000 katika majimbo sita ya uchaguzi.

Wakati huo huo, DAWASA imetoa elimu kuhusu huduma zinazotolewa na wakala kwa wakazi wa Vikawe Kata ya Pangani, wilayani Bagamoyo ikiwa ni pamoja na kuwahamasisha kujiunga na huduma mara baada ya kukamilika kwa mradi mkubwa wa maji kutoka Makongo hadi Bagamoyo.

Akizungumza na wakazi hao, Ofisa Biashara Mkoa wa kihuduma DAWASA - Mapinga, Christopher Sika, aliwahimiza wananchi walio karibu na mtandao wa maji waendelea kuleta maombi ya maunganisho ya huduma kwani uhakika wa huduma hiyo ni mkubwa.

"Mradi umekamilika na huduma inapatikana katika eneo letu, nitumie nafasi hii kuwaomba wananchi wazidi kujitokeza kwa wingi kuleta maombi ya kuunganishwa ili tuwapatie huduma ya majisafi,"alisema Sika

Aliongeza kuwa wananchi wote wanaopata huduma ya maji kuendelea kulipia ankara za matumizi ya mwezi kwa wakati ili fedha hizo zitumike kuboresha na kusogeza huduma kwa wananchi wengine wenye uhitaji.

Naye Mwenyekiti wa Kitongoji cha Vikawe, Jihadhari Mindawa, aliishukuru DAWASA kwa elimu na ushirikiano mkubwa wanaotoa kwa wananchi kwasababu hadi sasa huduma ya maji ni nzuri katika eneo hilo.

"Tunashukuru sana kwa elimu hii na tunawaomba DAWASA waendelee kutoa huduma bora kwa wananchi nasisi tutaonyesha ushirikiano mkubwa kwao katika kulinda miundombinu ya maji," alisema.

Mkazi wa Vikawe, Aminatha Michael alipongeza utaratibu wa utoaji elimu kwa wananchi kwani huwa unawakumbusha mambo mengi ikiwepo wajibu wao baada ya kupatiwa huduma.

Eneo la Vikawe bondeni ni mojawapo ya wanufaika wakubwa wa mradi wa uboreshaji wa huduma ya maji kutoka Makongo hadi Bagamoyo uliotekelezwa kwa gharama za shilingi bilioni 65 na unaohudumia kata za Mapinga, Pangani na Kerege.

# Sekta binafsi yahimizwa kushiriki kupinga ukatili

**Na Frank Monyo**

MTANDAO wa Kupambana na Ukatili wa Kijinsia (MKUKI), wamehimiza sekta binafsi kushirikiana na asasi zisizo za kiserikali kwa kutenga fedha kwa ajili ya kubuni utekelezaji mikakati na mbinu za kutokomeza ukatili wa kijinsia nchini.

Hayo yamesemwa jana mkoani Dar es Salaam wakati wa uzinduzi wa Maadhimisho ya Kampeni ya Siku 16 za Uanaharakati Dhidi ya Ukatili wa Kijinsia na wadau wa mtandao wa MKUKI unaojumuisha mashirika yasiyo ya kiserikali zaidi ya 200 chini ya uratibu wa Shirika la Wanawake katika Sheria na Maendeleo barani Afrika (WiLDAF) kwa kushirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Msaada wa Sheria (WLAC), Theodosia Muhulo alisema kuwa kwa upande wa Sekta Binafsi, MKUKI wanaimiza watenge fedha kwa ajili ya programu mbalimbali za kuzuia ukatili, ili kujenga taifa imara na salama ambalo litazalisha na kuongeza pato la nchi.

"Sekta binafsi zishirikiane na asasi zisizo za kiserikali katika kubuni na kutekeleza mikakati na mbinu mbalimbali za kutokomeza ukatili wa kijinsia. Kwa upande wa Taasisi za Dini, MKUKI tunahamasisha kuendelea kuwekeza katika kuzuia vitendo vya ukatili wa kijinsia kwa kuhusisha mafundisho ya dini na katazo za ukatili hasa katika kipindi cha kampeni na hata baada ya hapo," alisema.

Aliongeza kuwa taasisi za dini zishirikiane na wadau wengine katika kuripoti na kuchukua hatua pale wanapoona waumini wao wanafanyiwa vitendo vya ukatili wa kijinsia. "MKUKI inatoa pongezi kwa taasisi za dini ambazo zimetengeneza sera maalum za kuzuia ukatii wa kijinsia," alisema.

Mkurugenzi wa WilDAF, Anna Kulaya alisema kampeni ya siku 16 inatoa fursa kwa kila mwananchi kuwekeza kumaliza vitendo vyote vya kibaguzi na vinavyosababisha ukosefu wa usawa wa kijinsia, ndoa za ututoni na ukeketaji.

"Sote tunatambua kuwa ukatili wa kijinsia ni Janga. Ni tatizo kubwa si tu kwa Tanzania bali Dunia kwa ujumla. Kwa hapa Tanzania, ukatili wa kijinsia umeendelea kuwa tishio hivyo kuleta madhara makubwa kwa wanawake, watoto, familia, jamii, na taifa kwa ujumla. Ukatili dhidi ya wanawake unasababisha wanawake washindwe kushiriki kikamilifu katika majukumu yao binafsi, ya familia, ya kiuchumi, siasa na hata ngazi za maamuzi," alisema Kulaya.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Dk. Anna Henga, alisema Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) imetoa taarifa ya hali halisi ya ukatili dhidi ya wanawake ya mwaka 2022.

Alisema asilimia 27 ya wanawake wenye umri kati ya miaka 15 hadi 49 wameripoti kufanyiwa ukatili wa kijinsia. Vilevile utafiti umeonesha kwamba asilimia 61 ya wanawake walio katika mahusiano na ndoa hufanyiwa maamuzi na wenza wao.

Aliongeza kuwa ripoti hiyo inasema kuwa asilimia 39 ya wanawake walio katika mahusiano hufanyiwa ukatili na wenzi wao, ikiwa ni asilimia 18 ni ukatili wa kimwili na asilimia 12 ni ukatili wa kingono.

"Wanawake na wasichana wenye ulemavu wanakutana na ukatili mkubwa zaidi kwani wamekuwa wakitengwa, kubaguliwa na hivyo kuwafanya wasiweze kufurahia haki zao za msingi.

Vile vile ripoti imeonesha kuwa asilimia mbili ya wanawake walio katika mahusiano wamewafanyia ukatili wenza wao," alisema Dk. Henga na kuongeza kuwa;

"Visababishi vya ukatili baina ya wanandoa na wenza wao ni pamoja na unywaji wa pombe kwa asilimia 52 na wivu wa kimapenzi kwa asilimia 61," alisema.

Mkurugenzi wa Shirika la Miracle Corners Tanzania, Dk. Katanta Simwanza alisema ukatili wa kijinsia unamgharimu kila mmoja wetu katika jamii. Unazuia juhudi zetu kama taifa kuendelea na kufikia maendeleo endelevu.



# Mifereji ya taka yageuzwa dampo

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MKUU wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri ameonyesha kusikitikishwa na kitendo cha baadhi ya wananchi jijini hapa kugeuza mifereji sehemu ya kutupia takataka na kutishia kuwepo kwa mlipuko wa magonjwa ya kuambukizwa.

Shekimweri alisema ni jukumu la watendaji wa kata na mitaa wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma kuwahimiza wananchi kufanya usafi wa mazingira na kuondoa takataka hizo kila wakati badala ya kusubiri kufanyika kwa kampeni maalumu.

Alisema ni jukumu la viongozi hao na wananchi kuhakikisha mitaro hiyo inakuwa safi wakati wote kwa kuwa ndio wazalishaji wa taka hizo.

Akizungumza juzi baada ya kushiriki kwenye uzinduzi wa usafi wa mazingira uliofanyika Kata ya Madukani, alisema inasikitisha mifereji hiyo kugeuzwa sehemu ya kutupa taka huku viongozi hao wakishindwa kuchukua hatua kukabiliana na hali hiyo.

"Sijaridhishwa na hali ya mifereji iliyopo mitaa ya kata hii ya Madukani kutokana na kujaa takataka na chupa na kusababisha maji kukosa mwelekeo na kutoa harufu mbaya, " alisema.

Alisema hali hiyo inatishia afya za wananchi na kuwataka watendaji wa Jiji la Dodoma kuchukua hatua badala ya kusubiri kampeni za usafi wa mazingira kwa kuzoa takataka.

Mkuu huyo wa wilaya, aliwataka viongozi hao wa kata na mitaa kujenga utamaduni wa kufanya ukaguzi wa mazingira kwenye maeneo yao mara kwa mara badala ya kukaa ofisini kusubiri kupelekewa taarifa.

Vilevile aliuagiza uongozi wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma kuhakikisha wanatoza faini kubwa kwa watakaobainika kuchafua mazingira sehemu za kazi na makazi ya watu ili kukomesha tabia hiyo.

"Tumieni sheria zenu kuwatoza faini kubwa ili iwe fundisho kwa wengine, hatuwezi kuona mifereji ya kupitisha maji taka inageuzwa sehemu ya kutupia taka kama tulivyojionea wenyewe," alisema.

Mkuu wa Idara ya Mazingira wa Jiji hilo, Dickson Kimaro, alimtaka kila mwananchi wa Dodoma kuhakikisha anazingatia usafi wa mazingira kwa kuweka eneo lake katika hali ya usafi badala ya kusubiri kushurutishwa na viongozi.

Kimaro, alisema jukumu la usafi wa mazingira ni la watu wote, hivyo Jiji la Dodoma linatakiwa kuwa mfano kwa usafi na kuonya kuwa watakaoshindwa wachuku-

# Serukamba atatua mgogoro wakulima, wafugaji

**Na Thobias Mwanakatwe,** ITIGI

MKUU wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, ametatua mgogoro wa ardhi baina ya wafugaji na wakulima wa vijiji vitatu wilayani Manyoni uliodumu kwa takribani miaka 12 baada ya kuamuru kila kijiji kipange matumizi bora ya ardhi na kuwekewa mipaka.

Wakulima na wafugaji hao wa vijiji vya Doloto, Dang'welu na Itigi kwa kipindi hicho, walikuwa wakigombea eneo hilo lililoko Doloto kwa kila kijiji kudai ni mali yake kwa kuwa wanaishi kulizunguka na kusababisha kuzorota kwa shughuli za maendeleo.

Akizungumza jana na wananchi wa vijiji hivyo katika mkutano wa hadhara uliofanyika Doloto, akiwa ameambatana na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa, Serukamba aliamuru kila kijiji kipange eneo la malisho, kilimo na ujenzi wa makazi kwa kuzingatia mipaka iliyopo.

Serukamba alimwagiza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Itigi, John Mgalula, katika kipindi cha wiki mbili kusimamia na kuhakikisha kila kijiji kinatenga eneo la malisho, kilimo, kuwekewa mpaka na kutangaza kwenye mkutano wa wananchi.

"Kila kijiji kipange maeneo yake ya malisho yajulikane yawekewe mipaka na Kamishna wa Ardhi atengeneze hati miliki ya eneo, naombeni ndugu sisi wote ni Watanzania Mungu ametusaidia tumekutana hapa Itigi na vijiji vyetu vimepakana tuheshimu mipaka ya kila kijiji," alisema

Serukamba alisema serikali inawahitaji wakulima na wafugaji, hivyo hakuna sababu ya kugombana kwa kuishi kwa amani na utulivu.

Alionya kama kijiji kitatenga eneo dogo la kufugia na kikawa na mifugo mingi, watalazimika kuipunguza kwa kuuza kwa sababu hawataruhusiwa kwenda kulisha eneo la kijiji kingine.

"Tumeamua hivyo sababu umoja umewashinda sasa sisi hatutaki migogoro kwenye nchi yetu, nchi inaongozwa na sheria ya kuanzishwa vijiji ambazo zinapaswa kuheshimiwa.

Msizuie mtu akipita na ng'ombe eneo lenye mgogoro kwenda mfano mnadani," alisema.

Serukamba alisema kila mtu aishi kwenye kijiji chake na ikitokea anataka kuhamia kijiji kingine akapokelewa ni sawa, lakini haiwezekani aishi Doloto na kuchungia mifugo Dang'welu.

Mkazi wa Doloto, Khamis Sungu, alisema eneo la kijiji chao lina mwingiliano na vijiji vya Dang'welu na Itigi baada ya kuvamiwa na wenyeji kukosa mashamba na malisho.



Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, akizungumza wakati wa mkutano wa hadhara wa kutatua mgogoro wa wakulima na wafugaji wa vijiji vya Doloto, Dang'welu na Itigi, katika kijiji cha Doloto jana, akiwa ameambatana na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

# Ma-RC, wakurugenzi halmashauri waagizwa kuajiri maofisa habari

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAKUU wa mikoa na wakurugenzi wa halmashauri nchini wameagizwa kuajiri maofisa habari wa kutoa taarifa ya kazi zinazofanywa na serikali kwa wananchi kwenye maeneo yao katika kipindi hiki taifa linajiandaa kwa uchaguzi wa serikali za mitaa mwakani na Uchaguzi Mkuu 2025.

Agizo hilo lilitolewa jana na Naibu Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Dk. Festo Dugange katika mkutano wa Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, wakurugenzi wa halmashauri nane za mkoa huo na vyombo vya habari jijini hapa.

"Nawaagiza wakuu wa mikoa yote na wakurugenzi wa halmashauri kuhakikisha utoaji taarifa kwa wananchi kuhusu nini serikali yao imefanya liwe endelevu hasa wakati huu tunaelekea kwenye Uchaguzi wa Serikali za Mitaa 2024 na Uchaguzi Mkuu 2025," alisisitiza Dk. Dugange.

Alisema kama kuna ofisi ya mkoa au halmashauri haina ofisa habari zifanyike jitihada za kumpata hata kama hakuna bajeti kwa wakati huu kwa mkataba wakati mipango mingine ikiendelea kufanyiwa kazi.

Alisema maofisa habari wanatakiwa kushiriki katika vikao vyote vya mikoa na vya halmashauri ili maamuzi yanayotolewa yawafikie wananchi.

"Siyo anakuwepo ofisa habari ambaye hata vikao hashirikishwi ni lazima ashiriki, pia muwatafutie vitendea kazi vyenye uwezo ili watekeleze majukumu yao kwa mujibu wa taratibu zao," alisema Naibu Waziri huyo.

Alisema agizo hilo la utoaji taarifa kwa wananchi linapaswa kuwa endelevu kwa wakuu wa mikoa na wakurugenzi wa halmashauri zote 184 nchini.





# Biashara usafirishaji haramu watoto yazidi kupasua kichwa

**Na Rahma Suleiman**, ZANZIBAR

OFISA Mdhamini wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Hafidh Ali Mohammed, amesema bado jamii haijaelewa kuwa biashara haramu ya usafirishaji watoto ni uhalifu mpya wenye athari mbaya kwa mustakbali wa nchi.

Mohammed aliyasema hayo wakati akifungua kikao cha wadau wa kupinga usafirishaji haramu watoto kilichofanyika Mazizini Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja.

Alisema wanaojihusisha na biashara hiyo wameugeuza uhalifu huo kama njia mpya kujiingizia kipato bila ya kujali athari zake kwa watoto hao na jamii.

Alisema biashara hiyo ni udhalilishaji wa kijinsia kwa watoto kwa sababu wanafanyiwa vitendo ambavyo vinawaathiri kimwili na kisaikolojia kwa kubakwa, kulawitiwa, kupigwa na kutelekezwa.


Akiwasilisha ripoti ya utafiti juu ya biashara hiyo visiwani hapa, Mkuu wa Divisheni ya Hifadhi ya Mtoto, Shehe Ali Shehe, alisema kuna idadi kubwa ya watoto wanaoingizwa kwenye biashara hiyo.

Shehe, alisema katika utafiti waliofanya kwa majaribio katika Shehiya ya Chukwani, Mbweni, Kiembe Samaki, Nyamanzi, Dimani, Bweleo na Fumba wamegundua jamii inaichukukulia biashara hiyo kuwa ni suala la kawaida.

Alisema lengo la kufanya utafiti huo ni kutaka kujua ukubwa wa tatizo hilo, mwelekeo wa jamii, uelewa wa watendaji wa serikali ngazi za shehiya na juhudi kukabiliana nalo.

Alisema katika utafiti huo wamegundua kuwepo kwa wimbi la watoto wageni wanaoingizwa kinyemela na kutumikishwa kwenye biashara za kuuza miili yao.

Shehe, alisema ili kupunguza tatizo hilo lazima kuwe na nguvu kazi ya pamoja na mashirika ya Umoja wa Mataifa (UN) katika ofisi za Zanzibar badala ya Shirika la Kimataifa la Uhamaji (IOM) pekee.



Rais wa Zanzibar Alhaj Dk. Hussein Ali Mwinyi akizungumza na Waumini wa Kiislam, baada ya ibada ya swala ya Ijumaa katika Masjid Noor Kombeni, Wilaya ya Magharibi "B" Mkoa wa Mjini Magharibi jana. **PICHA: IKULU**

# Wizara yatangaza mpango maendeleo

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

WIZARA ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi imesema imepanga mpango mkakati kwa lengo la kuleta maendeleo ya haraka katika sekta ya uvuvi, mazao ya baharini, utafutaji mafuta na gesi asilia nchini.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk. Aboud Suleiman Jumbe, aliyasema hayo visiwani Zanzibar wakati wa ufunguzi wa warsha ya siku tatu juu ya maabara ya kuharakisha matokeo chanya kwa vipaumbele vya ajenda ya uchumi wa buluu.

Dk. Aboud alisema kupitia warsha hiyo kutasaidia kutengeneza mfumo wa uangalizi na kutoa taarifa kwa ajili ya kujenga viashiria ambavyo vitaleta mageuzi ya haraka ya utekelezaji wa vipaumbele vya uchumi wa buluu.

Alisema sekta ya uvuvi na mazao ya baharini imekuwa kwa kasi hadi kufikia asilimia 6.3 kwa mwaka kutoka asilimia 4.5 tangu Rais wa Zanzibar, Dk Mwinyi alipoingia madarakani na kuleta maendeleo ya uchumi wa buluu nchini.

Meneja wa Uchumi wa Buluu, Hamad Bakari Hamad, kutoka Taasisi ya Rais ya Kusimamia Utendaji wa Kazi Serikalini, alisema ushirikiano unahitajika kuisaidia jamii kufikia malengo ya uchumi wa buluu ya kupitia uvuvi mdogo na ukulima wa mwani katika kila eneo kisiwani Unguja na Pemba.

Washiriki wa warsha hiyo, walisema itasaidia kuweka vipaumbele kuleta maendeleo kwa wananchi wa Zanzibar.

# Watakiwa kusajili nyimbo COSOZA

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

TAASISI ya Hakimiliki Zanzibar (COSOZA) imewataka watunzi wa nyimbo za injili kusajili kazi zao ili kufanya kazi zao kwa mujibu wa sheria na kudhibiti wizi wa kazi zao.

Akizungumza katika mafunzo ya kuwapatia uelewa wanachama wa nyimbo hizo katika Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Mwanakwerekwe, Mwanasheria wa taasisi hiyo, Zuhura Salum Juma, alisema hatua hiyo itawasaidia kubaki salama kwa kutoibiwa kazi zao na kuondokana na migogoro.

Alisema kuna watuwamekuwa wakiharibu Tasnia ya Muziki nchini, ikiwemo nyimbo za injili huku wakijua kuwa siyo wamiliki halali kwa lengo la kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu.

Alisema wasanii hunufaika na kazi zao kiuchumi iwapo watajiunga na COSOZA na kutambulika kisheria na kupatiwa mirabaha kila muda unapofika kwa ajili ya kazi hizo.

Alionya kuwa ni kosa kisheria msanii wa nyimbo au kazi yoyote ya ubunifu kuchukuliwa na mtu mwingine bila ya ridhaa ya muhusika na kufanya hivyo ni kosa kisheria.

Mkuu wa Divisheni ya Usajili COSOZA, Halima Ame Wadi, alisema kazi ya kutoa mirabaha inafanyika kwa mwaka mara moja, hivyo ni wajibu kwa wanachama na wadau wa injili kuwa tayari kusajili kazi zao ili kunufaika kiuchumi.

Alisema COSOZA inasajili kazi za msanii ili kuhakikisha zinalindwa na kuwa salama wakati wote.

Mkuu wa Kitengo cha Elimu na Uhusiano wa COSOZA, Iddi Makame Simai, alisema kazi ya msanii inaposajiliwa inapata ulinzi kwa mujibu wa sheria na kunapotokea sitofahamu ya kuibiwa au kupotea, inakuwa rahisi kupata haki yao.

Alisema suala la ulinzi wa hatimiliki ni ngumu kwa sababu nyimbo hupigwa nchi mbalimbali, hivyo nchi ikaona ipo haja ya kuweka sheria hiyo ya usajili kukabiliana na wizi wa sanaa na kumsaidia msanii kunufaika.

Mwinjilisti wa KKKT Mwanakwerekwe, Leah Gadi Koda, alisema imewasaidia kujua umuhimu wa kusajili kazi hizo ili kuepuka usumbufu wa kazi hizo kutumika katika maeneo mengine na kupoteza uhalisia na malengo ya kazi hizo.



**SIMI AMJIA JUU MCHUNGAJI** UKURASA 14

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI TELE





# MLETE WAMUONE

MWIGIZAJI Mkongwe wa Bongo Movie, Fridah Kajala Masanja tayari ameweka wazi kwamba amempata mwanamume wa shoka atakayeziba penzi la mwanamuziki Harmonize.

Katika kuonyesha kwamba hatanii katika suala hilo, amewaambia mashabiki wake kukaa tayari kupokea mwaliko wa harusi yake ya pili.

Hata hivyo, mwanaume aliyenaye kwa sasa si mtu maarufu, na amefanya hivyo kwa kile alichosema amepata fundisho kwa Harmonize, hivyo hawezi kurudia tena kosa hilo.

Hata hivyo, watu wengi wana wasiwasi na tangazo hilo kwani linaonekana kama mwendelezo wa majibizano ya kuumizana kati ya mastaa hao.

Baadhi ya mashabiki wake amesema kama Kajala alitaka kumsahau Harmonize, hakupaswa kutaja jina la mwanamuziki huyo kwani angefanya mambo yake kimya kimya.

"Unataka kuendeleza majibizanmo ya kuumizana, Kajala bado anampenda Harmonize na ndio maana anataja jina lake licha ya kumpata mwanaume mwingine," amesema.

Aidha, Asha Shabani amesema anachofanya Kajala ni kujituliza moyo kwa kigezo cha kuwa na mwanamume mwingine na akamshauri kama kweli ameingia katika uhusiano mwingine ni vyema akamuweka hadharani ili kila mtu amjue.

Kajala akiongea hivi karibuni alimpamba vilivyo mpenzi wake wa sasa akisema ametimiza vigezo vikuu ambavyo ni mwanaume kamili na sio mtu maarufu.

"Ni mwanamume kamili, yule ambaye nilikuwa namhitaji, nina vigezo vyangu lakini kwangu mimi yule ni asilimia 100. Moja ni kutokuwa maarufu, pili anamcha Mungu na tatu ni siri yangu mwenyewe," alisema Kajala.

Kajala na Harmonize waliachana mwishoni mwa mwaka jana na kuibua majibizano makali mitandaoni kwa kila mmoja akimtuhumu mwenzie kuwa chanzo cha kuachana kwao.

BASI SAWA

## Alenga awakata kiu 'Wrong Decision'

MWONGOZAJI na mwigizaji kutoka Houston Texas nchini Marekani, Elize Alenga maarufu kama Alenga The Great, amekata kiu ya mashabiki baada ya kuachia filamu yake mpya inayoitwa Wrong Decision.

Alenga ambaye ni mwongozaji wa filamu za kiswahili nchini Marekani, amewekeza fedha nyingi kwenye uzalishaji wa filamu ili kukuza tasnia na kuibua vipaji vipya.

Akizungumza na BT hivi karibuni, Alenga amesema filamu hiyo iliyotoka Jumamosi wiki hii imebeba simulizi ya kipekee ambayo imechezwa na waigizaji wenye vipaji vikubwa wakiongozwa na yeye mwenyewe.

"Naishukuru sana timu yangu, Gabby na James kwa kufanikisha filamu ya Wrong Decision, ni sinema nzuri yenye ujumbe mzuri," amesema



## Dudu baya kachafua tena



RAIA wa Kenya, Emanuel Omondi amesema msanii wa muziki wa Bongofleva Dudubaya amewadanganya Watanzania kwamba yeye ni meneja na promota wake.

Amesema mwanamuziki huyo ni shabiki wake na alikutana naye akiwa mgonjwa na alimhudumia na kumsaidia matibabu mpaka akapona maradhi yake.

"Mimi nilikuja kumsaidia kama msamaria mwema, nilimchukua na kumpeleka hospitali mjini Morogoro alitibiwa mpaka akapona. Lakini nimeumia kwa kuwadanganya watu kuwa mimi ni meneja wake na kaka yake, huyu ni muongo amenipa wakati mgumu hata nyunbani wananiuliza kama nimejiingiza katika muziki," amesema Omondi.



## DR CHENI ASIMULIA MAPITO YAKE

MWIGIZAJI na mshereheshaji maarufu, Dr Cheni amesema ametoka mbali na kazi yake ya usemaji katika sherehe mbalimbali kiasi ambacho alilipwa 5000 kama malipo yake.

Dr Cheni amesema kwa miaka 25 amekuwa na uvumilivu katika kuboresha kazi yake, lakini imekuwa na mabonde mengi mpaka sasa anapata mafanikio.

"Nilikuwa nawenda katika sherehe kama muhudhuriaji nilipewa 5000 kama nauli na posho yangu.Nilipoanza kuwa MC nilikuwa mgeni katika masuala ya ushereheshaji, sikujua kama fursa lakini nimepata mafanikio makubwa katika kazi yangu," amesem Dr Cheni.



## King Masaki ampa mama zawadi

MWANAMUZIKI wa kizazi kipya King Masaki, amesema wimbo wake mpya 'Zawadi Yako Mama' ni maalum kwa ajili ya kuwaenzi  wanawake wote nchini.

Amesema wimbo huo ambao amemshirikisha PNC katika kiitikio, umekuwa tofauti na nyimbo zingine kutokana na maudhui yake kumthamini na kumtukuza mwanamke ambaye ndiye anapitia wakati mgumu wakati wa kuzaa na kulea watoto.

"Hakuna nyimbo maalum kwa ajili ya zawadi ya mama ambaye ni muhimu, nikaona nitunge wimbo kwa ajili ya mama kuwapatia  zawadi na hii ni kwa ajili ya wanawake wote nchini," amesema King Masaki.

FILAMU

## Sijapoteza: Thamani ya mkia hadi ukatwe

**Na Adam Fungamwaango**

UPO msemo wa kiswahili kuwa mbuzi hajui thamani ya mkia wake hadi ukatwe. Maana ya msemo huu ni kwamba wakati mwingine binadamu hawezi kuona umuhimu au thamani ya kitu alichonacho, hadi kipotee, anyang'anywe au kiishe, ndipo anapotambua kuwa alichokuwa akikimiliki kilikuwa na umuhimu.

Leo tunaitazama iitwayo 'Sijapoteza'.

Imechezwa na wasanii Amri Athumani, maarufu kama mzee Majuto (marehemu), Mboto, na Getrude Mwakabana.

Inaanza kuonyesha kuwa Mboto na mkewe Salma, wanaishi kwa amani, wakiwa na mzee wao mzee Majuto ambaye ni baba wa Mboto.

Hata hivyo, tabia za Mboto na baba yake mzazi haziridhishi. Mboto ana tabia ya kupenda wanawake hovyo.

Waswahili wanasema mtoto wa nyoka ni nyoka, inawezekana kabisa kuwa tabia hii amerithi kutoka kwa baba yake, kwani mzee Majuto amekuwa na tabia hiyo hiyo.

Pamoja na utu uzima wake, amekuwa akitongoza wasichana wadogo ambao kiumri ni sawa na wajukuu zake.

Mashtaka na malalamiko yakawa hayakauki nyumbani kwao, lakini baba na mtoto wote akili zao ni sawa.

Baba na mwanaye wanatoka usiku kwenda kwenye vigodoro, kwa sababu tu eti ya kuangalia mademu wakali.

Siku moja Mzee Majuto anafumaniwa na mwanamke wa watu, waliomfumania wanampiga kidogo. Mzee Majuto tangu siku hiyo akajirekebisha.

Mambo yalizidi kuwa mabaya kwa Salma, alipoona mambo yanazidi, akaamua kuondoka.

Siku tatu tu tangu aondoke, tabu ikaanza. Kula ikawa tabu, Mboto akaona kabisa nyumbani kuna vitu vinapungua.

Ikabaki sasa kilio na kusaga meno. Mboto na mzee Majuto kila mtu akawa anamlaumu mwenzake kutokana na tabia mbaya.

Mboto akaamua aondoke hapo aende sehemu yoyote kuanza maisha mapya, kwani alijiona mpweke.

Katika hali isiyotarajia, mlango unafunguliwa na Salma anaingia. Wote wanashangaa. Anawaambia amerejea, kwani amewakumbuka na anampenda sana Mboto, ila ajirekebishe. Mboto anaomba radhi.




## BABA KALETA PANYA

**Na Adam Fungamwango**

KATIKATI, mpaka mwishoni mwa miaka ya 1990, kulikuwa na bendi zilizoundwa nchini ambazo hazikuwa kubwa sana, lakini zilivuma sana na kukonga nyoyo za mashabiki wa muziki wa dansi nchini.

Ikumbukwe bendi kama Juwata Jazz Band, DDC Mlimani Park Orchestra, Bima Lee, Maquiz Original, Orchestra Safari Sound (OSS), na zingine ndizo zilikuwa bendi kubwa kwa nyakati hizo ambazo nyingi zilianzishwa kuanzia miaka ya 1960 hadi 1980 katikati.

Leo tunakwenda kuziangalia bendi hizo ambazo zilivuma na kufa kifo kama mshumaa unavyozimika kwenye upepo mkali.

**Olduvai Band-Baba Kaleta Panya**

Ni bendi iliyokuwa ikipiga muziki wake kwenye Hoteli ya Sheraton jijini Dar es Salaam baada ya kuanzishwa mwaka 1996. Hakuna aliyekuwa anaifahamu hadi pale iliporekodi wimbo wake uliotokea kuwa maarufu uitwao, 'Ndumilakuwili.'

Mashabiki hawakuufahamu kwa jina hilo, bali waliuita 'Baba Kaleta Panya' kutokana na kuwa na baadhi ya maneno hayo ndani ya wimbo huo.

Ni wimbo uliokuwa na vibwagizo vilivyoufanya kuwa maarufu sana enzi hizo. Navyo ni hivi.

"Watoto hawa bwana kula wanakula, kuvaa wanavaa lakini lo, machangudoa."

Baba kaleta pungo baba kaleta pungo, we, uchicheme pungo chema mbuzi ya porini mwenye nyumba hii ni Mwichilamu, akitufundua atatupukucha turudi kwetu nchumbiji.

Baba kaleta mbwa baba kaleta mbwa, we usiseme mbwa, sema mbuzi ya kisasa, mwenye nyumba hii ni Mhehe, akitugundua atatunyang'anya.

Baba kaleta panya baba kaleta panya, we usiseme panya, sema samaki nchanga, mwenye nyumba hii ni Mmakonde akitugundua atatunyang'anya."

**Chezimba Band - Kijogolo Sina Nyumba**

Bendi hii ilikuwa ikipiga muziki wake Twiga Hotel Dodoma, ikiongozwa na Gerry Gumbo miaka hiyo hiyo ya katikati ya 1990.

Nayo ilirekodi wimbo ilioondokea kunyanyasa sana ulioitwa 'Kijogolo Sina Nyumba'. uliokuwa na mashairi yafuatayo.

"Kijogolo sina nyumba nitajenga barabarani, nikajenga nyumba ya mawe oo, ghorofa ndani kwa ndani, sijaona manowari oo, ikipita barabarani."

Walirekodi na mwingine uliovuma uliokuwa na maneno, 'Macho nyanya mshumaa useme utakacho nitakupa...'


**Africulture-Mahepe Ngoma ya Wajanja**

Ilikuwa ni bendi iliyoundwa na Marijani Rajab baada ya kufa kwa bendi ya Dar International. Jina la bendi yake halikuvuma sana, lakini mtindo aliotumia wa 'Mahepe Ngoma ya Wajanja', ndiyo uliowaacha hoi mashabiki na kusababisha bendi ivume.

**Salna Six Brothers-Fitina**

Bendi hii ilikuwa na maskani yake mjini Tanga. Ilivuma sana na wimbo wake wa 'Fitina' ambao uliwawezesha kushika nafasi ya pili kwenye mashindano ya bendi bora miaka hiyo ya 1990 iliyoitwa MASHIBOTA.

**Makondeko Six Band-Kila Munu Ave na Kwao**



Ilimilikiwa na mwanasiasa, mfanyabiashara, msomi na mbobevu kwenye masuala ya muziki Dr. Alex Khalid.

Alikwenda kumng'oa Harila Tongolanga toka CTU Les Mwenge na kumpa uongozi na kutikisa nchi, lakini nayo ilijifia ghafla.



# Made Kuti apata jiko

MWANAMUZIKI wa Afrobeats kutoka Nigeria, Omorinmade Kuti, maarufu kama Made Kuti, amefunga ndoa na mpenzi wake wa muda mrefu.

Mkali huyo wa muziki ambaye ni mjukuu wa mwanamuziki mkongwe marehemu Fela Anikulapo Kuti, aliweka video katika ukurasa wake wa Instagram akionekana yeye na mke wake wakiwa katika hafla ya harusi akiwa amevaa suti safi na kumpiga busu mwandani mwake.

"Leo hadithi ya mapenzi iliyoanza na wahusika wawili inaendelea. Acha tukio lianze, tunashukuru kwa kupatana. Nimefurahi kutumia maisha yangu yote na wewe. Leo ni maalum kwa chakula cha harusi " ameandika Kuti.



## Tems akumbuka mahabusu Uganda

MWIMBAJI wa muziki wa Afrobeats kutoka Nigeria, Tems amesema amepata uzoefu wa ndani ya gereza wakati alipotiwa mbaroni nchini Uganda mnamo 2020.

Tems akiwa na msanii mwenzake Omah Lay, walikaa ndani ya gereza kwa siku mbili baada ya kukiuka sheria ya kudhibiti ugonjwa wa Corona.

Akizungumza wakati wa mahojiano ameeleza alikuwa katika gereza dogo, mwanzoni aliona kama mzaha lakini alipofika ndani alijua sio ndoto bali ni kweli na ndipo alipoanza kulia.

## Channing,Zoe wafunga ndoa

WASANII wa filamu kutoka Hollywood, Channing Tatum na Zoe Kravitz wanaripotiwa kuoana baada ya miaka miwili ya uchumba.

Kulingana na Jarida la People, vyanzo vingi vimethibitisha kwamba wanandoa hao walioana hivi karibuni.

Mnamo Oktoba 28, 2023, wawili hao walitoka pamoja ili kuhudhuria karamu ya Halloween ya Kendall Jenner, wakati ambapo pete ya uchumba ilionekana kwenye kidole cha Kravitz.

Wawili hao walikutana kwenye kazi ya uchukuaji picha ya filamu ya Kravitz inayoitwa Pussy Island na kila mmoja alionekana kumuwaza mwenzake kimapenzi.





## Ninolowo akana ukware

MWIGIZAJI wa Nollywood, Bolanle Ninolowo amekanusha kwamba maisha yake yametawaliwa na tabia ya ukware kupenda wanawake wengi.

Akiwa kwenye kituo cha TVC,amesema simulizi inayosambaa kwamba kutokana na sura yake ya kuvutia, huwa anawadanganya wanawake na kujihusisha nayo kimapenzi.

Amesema katika kipindi cha miaka mitano hadi saba ambacho ametumia kuigiza, hakujawahi kuripotiwa kuwa na uhusiano na mpenzi wala kujihusisha na ukatili wa kijinsia.

## Simi amjia juu mchungaji

MWANAMUZIKI maarufu Simi amepinga kauli ya mchungaji mmoja ambaye alitaka wanawake kuacha nywele zao halisi badala ya kuvaa wigi kichwani.

Muhubiri huyo wa kike alisema wanawake wanapaswa kujifunga na kuacha nywele zao za asili ili kuwavutia wanaume wa kuwaoa.

Kufuatia kauli hiyo, mwimbaji huyo aliingia kwenye akaunti yake rasmi ya Twitter, na kusema kiongozi huyo wa dini ameonyesha chuki kwa sababu wanawake wanajitahidi kujipenda wenyewe na wanatakiwa kuwa huru kufanya wanachotaka.





## TAWIRI yatetea utafiti kisayansi

**Na Daniel Sabuni,** ARUSHA

TAASISI ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania (TAWIRI) imesema tafiti za kisayansi zinazofanywa kupambana na wanyamapori wakali na waharibifu zinasaidia ujio wa matumizi ya teknolojia ya visukuma mawimbi na kurahisisha kuwafuatilia.

Wanyamapori waliofungwa visukuma mawimbi (GPS-Satellite Collars) nchini hadi sasa ni tembo ambao wanadhibitiwa kabla ya kuleta madhara kwenye makazi na mashamba ya wananchi.

Mkurugenzi Mkuu wa TAWIRI, Dk. Eblate Mjingo, aliyasema hayo jana jijini Arusha wakati akibainisha umuhimu wa tafiti za taasisi hiyo kuelekea mkutano wa 24 wa Kamisheni ya Afrika ya Misitu na Wanyamapori (AFWC24) na wiki ya nane ya Misitu na Wanyamapori Afrika (AFWW8).

Dk. Mjingo, alisema tafiti za wanyamapori zimekuwa chachu kutoa ushauri kwa serikali, mamlaka za hifadhi, watunga sera na wadau katika kuimarisha uhifadhi na kukuza utalii nchini.

Alisema teknolojia ya helikopta hutumika kurejesha makundi ya tembo hifadhini na kutoa elimu ya mbinu rafiki kwa wananchi wanaozunguka maeneo ya hifadhi ikiwa ni ujenzi wa maboma imara ya mifugo ya kuzuia wanyamapori aina ya kanivora kuvamia mifugo.

TAWIRI imeandaa Kongamano la 14 la Kimataifa na Kisayansi litakalofanyika kuanzia Disemba 6 hadi 8 mwaka huu kujadili pamoja na mambo mengine, maisha jumuishi baina ya binadamu na wanyamapori kwa uhifadhi wa baonuai na kwa maendeleo ya kiuchumi na ustawi wa jamii.

# Wanafunzi wapya waanza kwa maonyo

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

CHUO Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU), kimetoa ilani yenye maonyo 10 kwa wanafunzi 2,799 waliodahiliwa kuanza mwaka mpya wa masomo 2023/24 ili kuepuka kutimuliwa chuoni.

Akizungumza katika wiki ya mwongozo wa masomo kwa wanafunzi wa ngazi ya astashahada, stashaha na shahada ya kwanza, Makamu Mkuu wa MoCU, Profesa Alfred Sife, alisema kwa kuwa wamefanya chaguo sahihi la kujiunga na chuo hicho, ni vyema wanafunzi hao waliodahiliwa hadi jana kujiepusha na matukio yanayokinzana na sheria za chuo na kutimiza ndoto zao kwa kuhitimu masomo.

Kwa mujibu wa Profesa Sife, ni kosa kwa mujibu wa sheria za chuo mwanafunzi kwenda klabu za usiku, kujihusisha na ulevi wa kupindukia, wizi, kuvaa suruali chini ya kiuno, nguo fupi maarufu kama vimini, kupigana na kukosa vipindi darasani.

Kutojihusisha na utumiaji wa dawa za kulevya za heroin, cocain, bangi, mirungi na mapenzi ya jinsia moja (ushoga).

"Jitahidi sana ukiwa MoCu na Moshi kuishi maisha ya kitaaluma.

Muwe makini na maambukizi ya virusi vya ukimwi," alisisitiza.

Mkurugenzi wa Idara ya Huduma za Wanafunzi wa MoCU, Dk. Elisifa Nnko, alisema lengo la kusanyiko hilo ni kutimiza utaratibu wa chuo kuhakikisha wanafunzi wanaojiunga na mwaka wa kwanza wanapata fursa ya kuelezwa mambo mbalimbali.

"Tumeanza kwa kuwaeleza hiki ni chuo kikuu pekee cha Ushirika katika Bara la Afrika, misingi ambayo itawasaidia kufikia malengo yao na ndoto zao wawapo chuoni na raia wema na watumishi wema popote pale duniani," alisema Dk. Nnko.

Awali, Rais wa Serikali ya Wanafunzi MoCUSO, Yohana Kazimiri, aliwasihi wanafunzi hao wasikubali kuwa limbukeni wa kuiga mambo yasiyofaa na kuwataka kuishi maisha ya kawaida ili kutimiza malengo yao ya kupata taaluma bora.




Mkimbiza Mwenge wa Uhuru kitaifa mwaka 2023, Emmanuel Hondi kutoka Mkoa wa Manyara (katikati), akilishwa keki na Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana (UVCCM) mkoa wa Manyara, Inyasi Ams (wapili kulia), wakishirikiana na Mwenyekiti wa UWT mkoa, Fatuma Tsea (kushoto), Mwenyekiti wa UVCCM wilaya ya Babati, Magreth Uronu (wapili kushoto) na Katibu wa UVCCM mkoa, Ashura Kizigo, wakati wa hafla ya kumpongeza mjini Babati juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Shirika kukata rufani dhidi ya Mkurugenzi wa Mashitaka

**Na Tumaini Mafie,** ARUSHA

SHIRIKA la CILAO linalojishughulisha na utoaji wa elimu ya uraia na msaada wa kisheria, linatarajia kukata rufani mahakamani kupinga uamuzi wa Mkurugenzi wa Mashitaka (DPP) kuwafungulia watu mashtaka bila kukamilika uchunguzi na kusababisha kusota mahabusu kwa muda mrefu.

Jana, Mkurugenzi Mtendaji wa CILAO, Charles Odero, aliliambia Nipashe kuwa uamuzi huo unatokana na kutopendezwa na hukumu iliyotolewa Disemba 19 mwaka 2022 na Mahakama Kuu, Kanda ya Dar es Salaam katika kesi namba 20 ya mwaka 2021.

Kesi hiyo awali ilifunguliwa Mahakama Kuu, Kanda ya Tanga, kabla ya kuhamishiwa Dar es Salaam, CILAO wakilalamikia watu kukamatwa na kufunguliwa kesi bila kukamilika uchunguzi.

Kutokana na kutopendezwa na hukumu hiyo, jopo la wataalamu na wanasheria wao walikaa na kushauri kukatwa rufani. Kwa mujibu wa Odero, CILAO ilipeleka ombi la kufungua kesi hiyo ya rufani Septemba 26 mwaka huu kwa kuwa lina maslahi ua umma na ni haki inayomgusa kila mtu.

Iidai wanachopigania ni kuwepo kwa mifumo bora ya utoaji haki na kwa wakati badala ya mshtakiwa kusota mahabusu kwa muda mrefu kutokana na uchunguzi kutokamilika.

"Sheria yoyote inayomgusa mwanadamu, ukiwa wewe ni Mtanzania ukiona inakinzana ukainyamazia ni dhahiri itatuumiza sote.

"Kama siyo leo, ipo siku itakuja upande wako na itakulazimu uitumikie kwa maumivu.

Unakuta mtu anakaa rumande miezi sita, kwa kile kinachodaiwa kutokamilika upelelezi.

Watu wanakosa haki zao za msingi na kupoteza muda mwingi mahabusu, siyo sahihi na siyo haki," alisema.

TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA

# Yalipotokea maneno 'boi', 'taniboi' na 'konda'

**Na Adam Fungamwango**

UNAPENDA sana kunitumatuma kwani mimi boi wako?" Nadhani umeshawahi kusikia hili au kuambiwa na ndugu yako, au rafiki yako enzi hizo.

Hata mama zetu walipenda kulitumia hasa pale mtoto anarudi shuleni nguo zikiwa zimechafuka kupita kiasi.

"Unasikia, mimi siyo boi wako wa kukusugulia shati lako unalochafua kwa michezo yako ya kijinga huko shuleni." Baadhi ya kinamama walikuwa wakiwaambia watoto wao zamani.

Na neno hili limerithishwa kizazi hadi kizazi kwani hadi sasa, kinamama wa wakati huu ambao enzi hizo walikuwa mabinti wadogo wakifokewa na wazazi wao, nao wanalichukua na kulipeleka kwa watoto wao pia.

Ndiyo maana mpaka sasa neno 'boi' bado linatumika. Na kwa tafsiri ambayo wengi wanaifahamu boi ni kama mtumwa, mfanyakazi, lakini siyo ule wa kawaida, bali ni kutumwatumwa mara kwa mara bila kupata muda wa kupumzika.

Hata hivyo si wengi wanaofahamu asili ya neno, limetokea wapi na kwa nini limenasibishwa na mtu anayetumwa sana.

**BOI**

Hili ni neno lililotoholewa kwa toka lugha ya Kiingereza liitwalo 'boy', likiwa na maana kijana au mvulana.

Wazungu, Wajerumani na Waingereza kila mmoja kwa wakati wake walipoingia nchini walihitaji watu wa kuwasaidia kuanzia maofisini, mashambani, hadi majumbani.

Kwa maana hiyo wanawachukua wazawa na kuwapa kazi kwenye maeneo hayo yote.


Wale waliokuwa wakichukuliwa kufanya kazi kwenye majumba ya Wazungu, walikuwa wakiitwa hivyo na mabosi wao.

Wazungu hawakuwaita majina yao halisi, badala yake 'boy' wakiwa na maana kijana.

Kwa sababu kila kijana aliyekwenda kufanya kazi za ndani kwa Mzungu aliitwa kwa jina hilo, basi wazawa kwa sababu hawakujua lugha wakadhani ni msamiati wa wafanyakazi wote wanaofanya kazi kwenye nyumba za wazungu.

Na kwa ujumla kazi zao ilikuwa ni kutunza bustani, kupiga pasi, kufua nguo, kutunza nyumba na wakati mwingine mpaka kupika.

Sasa kwa sababu Wazungu walikuwa wakiwaita kwa jina hilo halafu wanawatuma kufanya hiki na kile, Wabongo wa wakati ule kabla ya Uhuru, wakaunganisha tu mtu anayetumwa anaitwa boi.



Pichani ni mabasi ya enzi hizo kipindi cha Mkoloni, mbele ya basi chini kidogo inaonekana chuma kilichojitokeza kiitwacho hendeli, ambacho kilitumika kuzungushwa kama stata ili basi liwake, na kazi hiyo ya kutumia nguvu ikifanywa na Waafrika, hivyo kupewa jina la 'tanboi' na wenzao walipokuwa wakiwasikia wazungu waliwahimiza wazungushe.



Yoyote anayefanya kazi nyumbani kwa mzungu wakamwita 'boi la mzungu'.

Huko vijijini na mitaani wakalichukua rasmi neno hilo. Ukimtuma sana mtu atakuuliza tu.

"Wewe bwana unanituma sana kwani mimi boi wako?"

**TANIBOI**

Asili ya neno hili haitofautiani sana na ya kwanza. Kasoro yake ni kwamba 'Taniboi', yeye hayupo nyumbani kwa mzungu, bali kazini na hasa kwenye magari.

Limetokana na neno la Kingereza, 'turnboy.' Wazungu kama kawaida yao, walipenda kuwachukua Waafrika kama wasaidizi, au wafanyakazi hasa maeneo yanayohitaji nguvu zaidi.

Kwenye sekta ya usafiri, wazungu walikuwa na mabasi yao au malori ambayo kwa teknolojia ya wakati huo ikiwa chini sana kabla ya uhuru, magari mengi hasa makubwa hayakuwa na stata, yaani gari inawaka kwa kutumia ufunguo na mtu yumo ndani.

Badala yake magari yalikuwa yakiwashwa nje, eneo ambalo kuna bampa, na ilibidi kitumike kifaa kinachofanana na spana kubwa iliyojikunja mara tatu.

Kifaa hicho, kinakwenda kuchomekwa eneo la katikati ya bampa kulikozungushiwa duara ya njano. Ili gari iwake enzi hizo za mkoloni lazima uzungushe hicho kiduara kilichojitokeza katikati ya bampa, na ili izunguke ilibidi kutumia kifaa hicho cha hendeli.

Madereva enzi hizo walikuwa wazungu na wasaidizi walikuwa ni vijana wa kiafrika wenye nguvu hivyo ili gari iwake na kuondoka mzungu humwambia kijana kuwa, "turn boy, turn boy" yaani "zungusha kijana, zungusha kijana".

Kwa kuwa babu zetu enzi hizo Kingereza kiliwapiga chenga kwa sababu ilikuwa ni lugha ngeni basi wao lile neno 'turn boy', wakajua labda vijana wote wa Kiafrika wanaofanya kazi kwenye magari wakiwasaidia wazungu, wanaitwa 'taniboi.'

Kuanzia kipindi hicho hadi leo hii kijana yeyote aliyefanya kazi ngumu kwenye magari aliitwa kwa jina hilo.

**KONDA**

Msamiati wa konda, nao unatokana pia na neno la Kingereza liitwalo 'conductor.'

Watu wa aina hii walikuwa wakifanya kazi ya kukatisha tiketi kwenye mabasi ya mijini.

Wao wanakuwa ndani ya mabasi au nje, kazi yao ni kuchukua pesa na kumpa abiria tiketi ambayo baadaye huenda ikatakiwa kwa kukaguliwa na mtu mwingine aitwaye 'inspector' kwa kiswahili mkaguzi.

Zamani makodakta walionekana sana kwenye mabasi ya umma, Dar es Salaam, maarufu kama UDA, wakiwa na mashine za kutolea tiketi pamoja na mkoba wa kuwekea pesa.

Kuna wakati walikuwa wakikatishia ndani ya mabasi kwa kutembea akikusanya pesa kama makonda wa daladala, halafu wakaanza kukatishia nje kipindi cha foleni, kila anayefika kwenye mlango na kutaka kupanda, anakatiwa na kuingia ndani ya basi.

Halafu kuna mabasi yaliletwa nchini ambapo kondakta alikuwa na kizimba chake amekaa, kila anayepanda ni lazima apite pale kwanza kwenye kizimba kile, akate tiketi na kwenda kukaa kwenye siti.

Yalipoanza kuingia mabasi binafsi ya kubeba watu, yaani daladala, watoto wa mjini nao wakawabadilisha majina makondakta wa daladala. Wakawakatisha na kuwaita makonda.

**Tuma meseji 0716 350534**



# Israel yaongeza mashambulizi Gaza, 14,000 waliokimbilia hospitalini hatarini

**GAZA,** PALESTINA

MAPIGANO makali yanazidi kushika kasi Ukanda wa Gazi, jana pekee Israel imeshambulia maeneo matano tofauti kwa kutumia anga, majini na ardhini.

Jeshi la Israel lilieleza jana kwamba makombora yalilenga maeneo hayo kwa kutumia ndege, meli na vifaru ambavyo vimezingira eneo hilo.

Hata hivyo, Hamas walitoa taarifa yao kuwa wanapambana na jeshi la Israel kwa kutumia makombora yanayorushwa na vifaru.

Mashambulizi hayo ya anga yaliendelea usiku kucha wa kuamkia jana karibu na Hospitali ya Al-Quds iliyoko Mji wa Gaza ambako ndani kuna watu 14,000 ambao wamejihifadhi kulinda usalama wao.

Uongozi wa hospitali hiyo ulisema watu wanane waliwekewa mashine kwa ajili ya kuokoa maisha yao na haikuwezekana kuzisogeza kwa sababu barabara nyingi karibu na hospitali hiyo zimeharibika.

Ulisema mapigano makali na Hamas yalikuwa yakitokea umbali wa mita 500 kutoka hospitalini hapo. Israel inadhibiti barabara zote mbili ikiwa njia kuu za kutokea Gaza kaskazini na barabara ya pwani na kusababisha watu kutoka nje ya Gaza inakuwa vigumu kwa kuhofia kuhatarisha maisha yao pale wanapotaka kuondoka kuelekea kusini.

Theluthi mbili ya wakazi wa eneo hilo wanapata misaada michache inayotokea Misri.

Malori 300 na mengine 100 yalitarajiwa kuingia jana, ingawa hali katika eneo hilo ni ngumu na ya kutisha.

Zaidi ya watu 700,000 wanaoishi Gaza hawana umeme, maji wala mtandao.

Katika hatua nyingine, Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani Antony Blinken amefanya ziara yake ya pili nchini Israel kwa ajili ya kuipa shinikizo la kusitisha mapigano ili misaada iwafikie wakazi wa Gaza.

Safari yake pia itazingatia zaidi hatua za kupunguza madhara kwa raia wanaoishi Ukanda wa Gaza. Kabla ya kuondoka kwake, Blinken alisema atatafuta hatua madhubuti kutoka kwa Israel ili kuhakikisha kuwa madhara kwa raia wa Palestina yanapungua.

Alisema Rais wa Marekani Joe Biden pia alitoa wito wa kusitishwa kwa vita kwa muda kwa ajili ya kupeleka misaada ya kibinadamu huko Gaza.

Ziara hiyo inafuatia kauli ya Israel iliyotolewa Alhamisi jioni kuwa jeshi lake lilikuwa limeuzingira kabisa mji wa Gaza na lilikuwa likishiriki katika mapigano ya ana kwa ana na wapiganaji wa Hamas.

Aidha Marekani imerusha ndege zisizo na rubani Ukanda wa Gaza kuchunguza sehemu ambalo mateka wa Israel wamewekwa.

Maofisa wawili wa Marekani walisema kwa mujibu wa tovuti ya Middle East Eye, kwamba Marekani inarusha ndege zisizo na rubani za upelelezi juu ya anga la Gaza.

Ndege hiyo ya MQ-9 Reaper, inayoendeshwa na Kikosi Maalum cha Operesheni cha Marekani, ilionekana kwenye tovuti ya ufuatiliaji wa safari za ndege za umma -Flightraider24.

Hata hivyo, Marekani ilisema kwamba ilianza kufanya kazi hiyo katika eneo la Gaza baada ya tukio la Oktoba 7, kulingana na gazeti la New York Times.

Israel inafanya safari za upelelezi mara kwa mara juu ya anga la Gaza, lakini ni mara ya kwanza kwa ndege zisizo na rubani za Marekani kutumika katika vita vya anga.

**BBC**

## Waafrika kuingia bila viza Rwanda

**KIGALI,** RWANDA

SERIKALI ya Rwanda imetangaza kuondoa viza kwa Waafrika wanaoingia nchini humo katika mkakati wake wa kukuza usafiri huru wa watu, biashara na utalii.

Hatua ya kuondoa visa kwa Waafrika wanaosafiri kwenda HYPERLINK "https://www.dw.com/sw/hrw-yaishutumu-rwanda-kwa-mauaji-ya-wakosoaji-nje-ya-nchi/a-67051224" Rwanda, ilitangazwa na Rais Paul Kagame juzi mjini Kigali.

Rais Kagame alilitaka bara la Afrika kuwa eneo moja la utalii, huku akisikitishwa kuona asilimia 60 ya watalii barani Afrika ni kutoka nje ya bara hilo, kulingana na data za Tume ya Uchumi ya Umoja wa Mataifa.

Akifungua mkutano wa kimataifa wa 23 wa baraza la utalii Duniani, Rais Kagame alisema Mwafrika yeyote, anaweza kupanda ndege kwenda Rwanda wakati wowote anapotaka na hawatalipa chochote kuingia katika nchi yake.

Kagame alisema kuwa katika dhamira ya kujenga upya taifa lake, nchi yake ilitambua utalii kama kichocheo kikuu cha ukuaji wa uchumi.

"Tulifikiria Rwanda ambayo mtu yeyote ulimwenguni angependa kusafiri kwenda.

Hivyo ndivyo, tulichagua utalii mapema na kuufanya kama kichocheo kikuu cha ukuaji wa uchumi na ajira. Na hatujakatishwa tamaa.", alisema Kagame.

Aidha, alisisitiza kwamba Waafrika watakuwa mustakabali wa utalii wa kimataifa katika miongo ijayo.

Kwa upande wake, rais wa Tanzania Samia Suluhu Hassan ambaye pia alihudhuria mkutano huo, alitoa wito kwa nchi za Afrika kuandika upya kuhusu bara hilo kwa kueleza simulizi zao wenyewe.

**DW**



Mwanajeshi wa Kenya akishika lindo wakati Mfalme Charles III wa Uingereza akitembelea kituo cha Wanamaji cha Mtongwe huko Mombasa juzi. **PICHA: REUTERS**

## Russia kuchimba madini Equatorial Guinea

**MOSCOW,** RUSSIA

RAIS wa Russia Vladimir Putin amesema kuwa kampuni kutoka nchini humo zinatarajia kuchimba rasilimali za madini ya Equatorial Guinea.

Kiongozi huyo alifanya mazungumzo na Rais wa Equatorial Guinea Teodoro Obiang Nguema siku ya Alhamisi mjini Moscow,na wote wawili walikubaliana kuimarisha uhusiano baina ya nchi hizo mbili. "Uwezo wa uwekezaji ni mkubwa, na uwezo wa nchi yako katika kuendeleza mahusiano haya pia ni mzuri," alisema Putin.

Alisisitiza "Ninamaanisha kuhusu uwezo zaidi unaohusiana na uchimbaji wa rasilimali za madini,"

Equatorial Guinea, nchi ndogo ya Afrika ya kati yenye utajiri wa mafuta, imejaliwa kuwa na rasilimali nyingi za madini kama vile dhahabu, almasi, urania na gesi.

Rais Nguema kwa upande wake alisema amezikaribisha kampuni za Russia zinazotaka kuwekeza nchini mwake.

Pia aliishukuru nchi hiyo kwa kufungua tena ubalozi wake nchini Equatorial Guinea.

**DW**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**BEATRICE EDWARD NELSON** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S0544/0009 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia MKUU SEKONDARI mwaka 2005. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/KIL/MWA/4203/2023.**

## KUPOTEA KWA VYETI



**PAYAS REUBEN MOREMI** anatangaza kupotea kwa cheti cha Chuo (Degrii ya Open University Tanzania) yenye namba 2407/T.96 iliyotolewa na **OPEN UNIVERSITY TANZANIA** mwaka 2000. Certificate in Law yenye namba 108/CLT/90 iliyotoelewa na **UNIVERSITY OF DAR ES SALAAM** mwaka 1993. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/MAG/RB/419435/2021.**

## KUPOTEA KWA VYETI



**EDINA ALBERT KASEBELE** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.1488.0009 kilichotolewa Baraza la Mitihani la Taifa kupitia ILOLO SEKONDARI mwaka 2014. Cheti cha chuo chenye namba S.1488.0009 kilichotolewa na MBALIZI INSTITUTE OF HEALTH SCIENCE mwaka 2016. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya **polisi: MB/RB/541/2019.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO MJINI**
**ILIYOPO MOROGORO**
**TANGAZO LA KUITWA SHAURINI**
**SHAURI LA MADAI NAMBA 224/2023**
**MDAI: SADOKI RAMADHANI MAKELE**
**DHIDI YA**
**MDAIWA: LUO XI**
**KWA; LUO XI**

**OMBI LA MDAI : MADAI YA PESA TSHS.550,000/=**
**MADAI YA PESA**

Unatakiwa kuhudhuria hapa Mahakamani katika shauri tajwa hapo juu bila kukosa.Shauri lilimepangawa kusikilizwa mnamo tarehe 09 Mwezi 11 Mwaka 2023 saa 2:30 Asubuhi .

Angalia kama hukudhuria/hamkuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu Mahakama ikithibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini, hii inaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa/mmeshindwa.

Hati hii yatolewa kwa Amri yangu na Chapa ya Mahakama hii leo tarehe 01/11/2023

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MOROGORO

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA RUFANI YA TANZANIA**
**DAR ES SALAAM**
**SHAURI LA MAOMBI YA MADAI NA. 511/17 YA 2020**
**VICENT MSANDA WAMBURA.............MUOMBAJI**
**DHIDI YA**
**KIPWELE.O. M. NDUNGULU .............MJIBU MAOMBI NA. 1**
**NURU OMARY LIGALWIKE................MJIBU MAOMBI NA. 2**
**EMILY T. KIRIA ..................................MJIBU MAOMBI NA. 3**
**SETTY OBEID MGAYA.......................MJIBU MAOMBI NA. 4**

**KWA,**
**KIPWELE.O. M. NDUNGULU**
**POPOTE ULIIPO**

Unajulishwa kwamba shauri la Maombi ya Madai tajwa hapo juu limepangwa kusikilizwa na Mahakama hii hapa Dar es Salaam tarehe 13/11/2023 saa tatu kamili asubuhi (9:00).
Unapaswa kuhudhuria siku na tarehe iliyopangwa bila kukosa na endapo hautahudhuria wewe mwenyewe au wakili wako anayetambulika kisheria rufaa itasikilizwa bila ya uwepo wako.
Imetolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 11/10/2023.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA KUU DODOMA**
**SHAURI LA ARDHI NA. 12 YA 2022**
**FATUMA SELEMAN BILALI..............................MDAI**
**DHIDI YA**

- **THE CITY COUNCIL OF DODOMA**
- **MOSES JACKSON MAKAPI**
- **ANA CHUNGU**
- **GAUDENSIA SAMSON MTATIRO**
- **EMMANUEL ANANIA**
- **MARIAMU KINABO**
- **COMMISSIONER FOR LANDS**
- **THE ATTORNEY GENERAL OF**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA............WADAIWA**

**KWA: 1. MOSES JACKSON MAKAPI**
**2. EMMANUEL ANANIA**
**3. MARIAMU KINABO**

**POPOTE PALE WALIPO**

**YAH: TAARIFA YA KUTAJWA KWA SHAURI LA ARDHI NA.12 YA 2022 MAHAKAMA KUU YA TANZANIA DODOMA.**

MNAFAHAMISHWA KWAMBA; Shauri tajwa hapo juu litatajwa Mahakama Kuu ya Tanzania Dodoma mbele ya MHE. A.J. MAMBI, JAJI wa Mahakama Kuu ya Tanzania Dodoma, saa tatu(3:00) kamili asubuhi siku ya jumatano tarehe 14/2/2024.
HIVYO; Mnatakiwa mfike nyinyi wenyewe au wakili wenu siku hiyo iliyotajwa bila kukosa.
NA ENDAPO; Hamtafika nyinyi au wakili wenu siku hiyo iliyotajwa inatosha kumaanisha kwamba shauri hili litashughulikiwa na Mahakama kama itakavyoamua pasipo nyinyi au wakili wenu kuwepo

IMETOLEWA; kwa mkono wangu na Mhuri wa mahakama leo hii tarehe 18/10/2023.

NAIBU MSAJILI

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA MOROGORO**
**MKOA WA MOROGORO**
**MAOMBI MADOGO NAMBA 111 YA 2023**
**KALOLY ANDEREAS MAHUMBU...............MLETA MAOMBI**
**DHIDI YA**
**JOSEPH ANJELO MOGELA.....................MJIBU MAOMBI**

**WITO/KUITWA SHAURINI**

**KWA**
**JOSEPH ANJELO MOGELA**

Popote ulipo unaarifiwa ufike katika Baraza za Ardhi na Nyumba la Wilaya ya Morogoro tarehe 15/11/2023 mbele ya mwenyekiti M .KHASIM wewe mwenyewe binafsi au utume muwakilishi wako bila kukosa ambapo maombi yamepangwa kutajwa.Endapo hautahudhuria maombi yatatajwa na kusikilzwa upande mmoja dhidi yako na kutolewa uamuzi.
Imetolewa kwa MKONO wangu na MUHURI wa Baraza leo tarehe 24 Mwezi Oktoba 2023.

M. KHASIM
MWENYEKITI

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SILAS CHARLES KIPEJA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye Namba za usajili **T. 261 ARC** Mitsubishi Fuso yenye Chasis no. **FK417J720782** Engine no. **6D16593861.** kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa polisi. RB Namba: **MWA/MAG/RB/558401/2021**

## KUPOTEA KWA PASSPORT



**ELENZIAN JOHN KOMBA** anatangaza kupotelewa kwa Hati ya kusafiria (Passport) yenye namba TAE098469 iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Makao Makuu mnamo tarehe 29/03/2019. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **DAR/STA/RB/922879/2023.**

**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Piga Simu 0677020701**

**OFISI ZA MATANGAZO Mikocheni Industial Area, Po.Box 31042, Dar es Salaam.**
**Mob: +255 - 0677020701**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**
**Website: www.ippmedia.com**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

MBWA mmoja wa jirani wa maeneo ya Kinondoni Msisiri, alionekana kuvutiwa na kiroba kilichotupwa upenuni mwa nyumba moja. Ni moja kati ya viroba ambavyo hutupwa usiku au alfajiri na vijana wanaokusanya taka kwenye nyumba za watu na kupewa ujira kidogo. Wao badala ya kwenda kutafuta maeneo ya kutupa, hupita vichochoroni na kama hajaonekana anautupa mzigo na kuendelea na safari yake. Ilitokea kwenye nyumba moja huko, na mbwa huyo alipouvuta, viungo vya mwili wa binadamu vilianguka. Majirani wa kwanza kuona walipiga kelele na watu wakajazana. Akinamama wakiangua vilio. Viungo vilihifadhiwa kwa kufunikwa. Polisi walianza msako. Kwa kuanzia tu wakaanza kuwakamata wazoa taka na waokota chupa za kwenda kuuza, wote wa maeneo hayo na jirani wanaofahamika tayari kwa mahojiano na uchunguzi, wakihisiwa kuwa huenda mmoja wao au zaidi kuhusika na mauaji. Ni maiti ya nani? Na Muuaji ni nani? Fuatilia mwanzo hadi mwisho kujua mkasa mzima ulivyokuwa.

## MAITI KWENYE KIROBA-33

**Na Adam Fungamwango : (0716 350534)**

"Kumbuka wakati unamtongoza Tessy, shoga yake Rukia huyo uliyekamatwa naye alikuwa anadhania kuwa yeye ndiye angechukua hiyo nafasi.

Kitendo cha kumuoa Tessy kilimuuma na alidhamiria kulipa kisasi na kuisambratisha ndoa ili aolewe yeye. Na hata alivyofanya hivyo, yeye alidhani utamuacha Tessy na kumchukua yeye. Ni kweli umemchukua, lakini ukaamua kufanya mauaji."

Hapo ndipo Charton aliposhtuka na kutambua mpenzi wake Rukia alikuwa amemdanganya.

Akaangua kilio mbele ya Eddy na askari kanzu waliompeleka pale.

"Ungefanya subira haya yote yasingekukuta, lakini ukaingiwa na wivu usio na maana, leo unakwenda kuhukumiwa kunyongwa hadi kifo kwa kumuua mkeo kwa sababu ambayo haikuwepo, ulidanganywa."

"Basi mke wangu anisamehe huko aliko, nilidanganywa. Kumbe Rukia ni mwanamke mbaya sana." Akalia na kuomboleza.

"Unamfahamu Nancy?" Eddy akamuuliza.

"Ndiyo." Akajibu huku akiwa ameshtuka.

"Ni nani yako?"

"Alikuwa mpenzi wangu, yaani mchepuko wangu wakati niko na mke wangu."

"Basi yeye ndiye aliyeniambia kila kitu. Na amefanya hivyo kwa hasira baada ya kumuacha na kumchukua Rukia, wiki chache baada ya kumuua mkeo."

Hata hivyo Eddy hakumwambia Charton kuwa kwa sasa yeye ndiye aliyemrithi Nancy.

**********************************

Kutokana na jinsi ushahidi wa kesi hii ulivyochukuliwa na Charton kugundua kuwa alidanganywa na Rukia na kujutia, wala haikuwapa shida majaji kwa sababu watuhumiwa wote walikiri mashtaka.

Umati wa watu ulifurika Mahakama Kuu wakati watuhumiwa wao wote watatu walipopelekwa mbele ya majaji watatu kujibu shtaka la mauji, kila mmoja akisomewa jinsi alivyoshiriki.

Charton ndiye wa kwanza kukiri, akisema alimuua mkewe kikatili kimakosa baada ya kudanganywa na mshtakiwa namba tatu, Rukia kuwa marehemu Tessy ni msaliti kwenye ndoa, alipomuonyesha picha ya mwanaume, lakini kumbe ilikuwa ya miaka mingi kabla ya kuwa naye.




**"Sijaona ukilia, mpenzi wako Barton kahukumiwa kunyongwa."**

Charton akakiri kumkodisha jambazi sugu Tinga Patauli ili kumuongoza jinsi ya kumuua binadamu huku akipitia mateso makali.

Akakiri kuwa walikuwa wakimkata viungo wakati marehemu yupo hai, hivyo mkewe akapitia maumivu makali. Kwa wakati huo yeye hakujali kutokana na kujawa na wivu wa mapenzi akidhani ni kweli mkewe ni msaliti.

Akawaambia majaji kuwa alihabarishwa na mpelelezi aliyekuwa akipeleleza kesi hiyo, Eddy Kamal kuwa Rukia alimdanganya kwa sababu tangu miaka ile alipokuwa akimchumbia Tessy, yeye ndiye aliyekuwa anataka kuchukua nafasi hiyo. Kwa hiyo hicho kilikuwa kama kisasi.

Na kweli Rukia alifanya hivyo akidhani atapewa talaka na kuolewa yeye, bila kujua kuwa aliamsha hisia kali zenye maumivu kwenye moyo wake.

Ni kweli Rukia alichukua nafasi ya Tessy, lakini penzi hilo halikudumu kwa sababu tayari limedhulumu nafsi ya mtu mwingine.

Siku ya hukumu iliwadia. Watu walijazana mahakamani kutaka kujionea wenyewe ni kitu gani kitatokea.

Pamoja na kukiri wenyewe hadharani kutokana na kwamba hawakuwa na njia yoyote ya kutokea kutokana na ushahidi usio na shaka uliotokana na upelelezi wa hali ya juu kutoka kwa Eddy Kamal.

Majaji wakaamua ifuatavyo. Mshtakiwa namba mmoja kwa sababu yeye ndiye mhusika mkuu na aliyemuua ni mkewe, alihukumiwa kunyongwa hadi kufa.

Mshtakiwa namba mbili hukumu yake ilikuwa sawa na mshtakiwa namba mmoja kunyongwa hadi kufa, kwa sababu wote wawili walimchukua marehemu wakampeleka kwenye jumba la mateso Ukonga Banana, akaanza kumtesa na kumkata kiungo kimoja baada ya kingine akiwa hai, wakimlazimisha amtaje mwanaume huyo. Licha ya kuwaambia hakuwa na bwana, waliendelea kumpa mateso makali, bila hata kumuonyesha picha ile. Ingewezekana angeweza kuitolea ufafanuzi, lakini marehemu alikufa bila kujua kisa kilichosababisha mateso yake ni picha ya zamani aliyopigwa na bwana yake Barton miaka mingi nyuma kabla ya kuwa na mumewe.

Mshtakiwa namba tatu, mke mtarajiwa wa Charton, Rukia, alihukumiwa kwenda jela miaka 15 kwa kutokana na kwamba yeye ndiye msababishaji mkuu wa yote yaliyotokea. Alichofanya ni kuchochea wivu na chuki kwa Barton ili amchukie mkewe. Hakunyongwa kwa sababu hakuua.

Wananchi walilipuka kwa hoi hoi na shangwe wakisema haki imetendeka. Ndugu, jamaa na marafiki wa Tessy walikumbatiana kwa furaha iliyochanganyikana na huzuni mahakamani hapo. Wale wa Barton, Patauli na Rukia wakaangua vilio.

**************************

"Mwanaume muongo wewe."

"Nani?"

"Wewe hapo."

"Nimekuongopea nini?"

"Ukanidanganya kuwa wewe unaitwa Denis."

"Kumbe?"

"Eddy Kamal, mpelelezi maarufu nchini. Nimekusoma sana kwenye vitabu na taarifa mbalimbali redioni. Nilidhania bonge la mtu kubwa kubwa, zee zee, kumbe hujai hata mkononi. Lakini wewee, kweli wewe ni mpelelezi maarufu, kumbe nakupa ubuyu wa Barton na Rukia kimapenzi tu, kumbe upo kazini!"

"Sijaona ukilia, mpenzi wako Barton kahukumiwa kunyongwa."

"Alinipiga kibuti, akamchukua Rukia baada ya kifo cha mkewe, mimi mwanzo nilijua nitchepuko wake ningechukua nafasi. Lakini kwa sasa sijutii tena, nipo na wewe, mtu maarufu. Yaani leo hii ndiyo nimejua."

Eddy na Nancy walikuwa wakitaniana baada ya hukumu hiyo Mahakama Kuu. Nancy ambaye siku zote hakujua mpenzi wake mpya ni nani, sasa ndiyo anatambua hivyo baada ya watu mbalimbali maarufu kumfuata na kumpongeza kwa kazi kubwa aliyoifanya kuipeleleza kesi hiyo kiasi cha kutowapa tabu majaji na mshtakiwa kulazimika kukiri wenyewe.

Eddy alimpitia Nancy nyumbani kwake na kwenda naye mahakamani hapo bila yeye mwenyewe kujua anapelekwa wapi. Alipofika akakutana na hicho alichokishuhudia.

"Yaani leo ndiyo nitalala kwa raha, usingizi mororo."

"Kwa nini?"

"Charton amepata haki yake, na mimi nimempata mwanaume ambaye sikutarajia hata siku moja kuwa naye. Eddy Kamal." Akalitaja jina kwa nguvu. Wakatazamana. Wakacheka. Wakakumbatiana kabla ya kuingia kwenye gari.

**MWISHO**

# BODI YA LIGI YAAHIDI DABI YA KISASA KESHO

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Bodi ya Ligi Kuu Tanzania (TPLB), umesema kesho itasimamia mechi ya Ligi Kuu ya watani wa jadi, Simba na Yanga kwa kufuata utaratibu waliyojifunza kupitia michuano ya Africa Football League (AFL ) iliyozinduliwa nchini mwezi uliopita.

Simba na Yanga zinatarajia kukutana katika mechi ya mzunguko wa kwanza itakayochezwa kesho kuanzia saa 11:00 jioni kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Bodi imekiri awali kulikuwa na changamoto mbalimbali kwa timu na mashabiki kabla na baada ya mchezo kufanyika.

Akizungumza na Nipashe jana, Ofisa Habari wa TPLB, Karim Boimanda alisema watasimamia mechi hiyo kwa kufuata utaratibu waliojifunza kupitia michuano hiyo ya kimataifa ambayo imeingia hatua ya fainali.

Boimanda alisema ili kurahisisha mashabiki kuingia mapema, mageti ya uwanja yatafunguliwa kuanzia saa 4:00 asubuhi na watahakikisha usalama unakuwepo ndani na nje ya uwanja.

"Tunakumbuka hivi karibuni tulikuwa na michuano ya AFL, tumejifunza mengi ikiwamo kuwapeleka watu wa usalama kambini kwa timu zote mbili na kupewa mtu maalum wa kuongeza msafara, timu zinakwenda mazoezini na kurudi siku moja kabla na siku ya mechi.

**Usalama wa mashabiki siku ya mchezo husika na kila aliyekata tiketi atakaa katika kiti chake, tumefuata utaratibu ule ule ambao ulifanyika katika AFL ," alisema Boimanda.**

Aliongeza wamefanya mazungumzo na mamlaka zinazosimamia usalama na wameahidi hali ya ulinzi utakuwa imara kwa sababu mchezo huo ni mkubwa na pia ni 'kioo' cha Ligi Kuu ambayo inashika nafasi ya tano barani Afrika na ulimwenguni ni ya 39.

"Usafiri maalum utakuwepo nje kwenda majumbani kwao baada ya mechi. Geti Kuu ni maalum kwa ajili ya magari tu, upande wa Kaskazini utatumia kwa ajili ya maofisa wa bodi, Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) na wanahabari, Kusini litatumika kwa ajili ya wadau wote waliopewa mwaliko.

Silaha za aina yoyote hazitakiwi katika mchezo huu na mwenye silaha anayemiliki kihalali basi anatakiwa kufika katika kituo cha polisi karibu na uwanja kukabidhi na baada ya mechi atafuata na kukabidhiwa mali yake," alisema Boimanda.

Yanga itashuka dimbani ikiwa ndio vinara na mabingwa watetezi wa ligi hiyo inayoshirikisha timu 16 kutoka mikoa mbalimbali hapa nchini.



Baadhi ya nyota na viongozi wa benchi la ufundi la JKT Queens wakiwa Ivory Coast tayari kushiriki fainali za Ligi ya Mabingwa Afrika kwa Wanawake. JKT Queens itatupa karata yao ya kwanza kesho kwa kuwavaa mabingwa watetezi, Mamelodi Sundowns Ladies ya Afrika Kusini. **PICHA: MTANDAO**

# Zimamoto FC kamili kuikabili KMKM

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MAAFANDE wa Zimamoto FC wamesema wamejipanga vizuri kuhakikisha wanaondoka na ushindi katika mechi ya Ligi Kuu Zanzibar dhidi ya KMKM itakayochezwa leo kuanzia saa 10: 15 kwenye Uwanja wa Mau A.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Zimamoto, Mohamed Hilali alisema anafahamu wanaenda kukutana na timu nzuri ambayo imesheheni wachezaji wazoefu wa ligi hiyo hivyo wataongeza umakini.

Hilali alisema katika mchezo huo amejipanga kucheza kwa kutumia mbinu tofauti ili kujihami na janga la kupoteza kutokana na kuwa na wachezaji wengi ambao ni majeruhi.

Kocha huyo alisema kama mwalimu tayari amezungumza na wachezaji na kuwajenga kisaikolojia kuacha kujiamini kupita kiasi na kutocheza kwa hofu.

"Tunacheza mchezo mgumu, na kila timu inapokutana na KMKM huwa inajiandaa sana kwa sababu tunaijua ni miongoni mwa timu nzuri, tumewaambia wachezaji kuacha hofu ya mchezo, kuacha kujiamini kupita kiasi, mambo haya yanaweza yakapelekea kupoteza mchezo," alisema Hilali.

Aliongeza kuhusu majeruhi aliokuwa nao katika kikosi chake baadhi wameanza kupona na watarejea uwanjani katika mechi ya mzunguko unaofata.

Zimamoto wanashuka dimbani wakiwa katika nafasi ya tano na alama 14 wakati wapinzani wao KMKM wakiwa kwenye nafasi ya pili baada ya kujikusanyia pointi 16.



# Singida, Namungo zakwama nyumbani

**Na Adam Fungamwango**

MPAKA kufikia raundi ya nane ya Ligi Kuu Tanzania Bara, Singida Fountain Gate na Namungo ndiyo timu ambazo hazijaonja ladha ya ushindi zikiwa kwenye mechi zao za nyumbani, imefahamika.

Mashabiki wa timu hizo wamekwenda uwanjani kuzitazama timu zao na kutoa hamasa katika mechi nne, lakini mechi zote wanaondoka kichwa chini kwa kukosa kupata matokeo ya ushindi baada ya dakika 90 kumalizika.

Takwimu zinasema Singida Fountain Gate imecheza mechi nne nyumbani kwenye Uwanja wa CCM Liti mkoani, Singida, ikitoka sare mara tatu na kupoteza mechi moja.

Timu hiyo ambayo zamani iliitwa Singida United ilitoka sare ya bila kufungana dhidi ya Prisons na baadaye Tabora United halafu ikichapwa mabao 2-1 dhidi ya Simba na Jumatano iliyopita ililazimishwa sare ya bao magoli 2-2 dhidi ya Ihefu.

Timu hiyo imecheza mechi nne ugenini ikishinda mbili na kupoteza mbili pia, ikiwafuata Mtibwa Sugar bao 1-0 Uwanja wa Manungu, Turiani, Morogoro na ikaikong'ota Namungo FC mabao 3-2, Uwanja wa Majaliwa, Ruangwa.

Kwa upande wa Namungo nayo haijapata ushindi wowote ikicheza kwenye uwanja wake wa Majaliwa, Ruangwa badala yake imetoa sare mbili na kupoteza michezo miwili katika mechi nne walizocheza.

Imechapwa bao 1-0 dhidi ya JKT Tanzania na mabao 3-2 dhidi ya Singida Fountain Gate, ikitoka sare bao 1-1 dhidi ya KMC na Mashujaa.

Namungo imeshinda mechi moja tu, ikicheza ugenini nayo ni ile ya Oktoba 27, mwaka huu dhidi ya Azam FC kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam ambapo ilipata ushindi wa mabao 3-1.

Imepoteza mechi moja ugenini na sare mbili kati ya nne ambazo imecheza nje ya uwanja wake wa nyumbani.

Ligi Kuu Tanzania Bara inatarajiwa kuendelea tena leo kwa Ihefu kuwaalika Azam FC kwenye Uwanja wa Highland Estates, Mbarali na kesho Simba itawakaribisha Yanga katika mechi ya watani wa jadi kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

## ZISIKUPITE

### JAMES ATAKIWA MADRID

KLABU ya Real Madrid inamtaka nahodha wa Chelsea, Reece James lakini The Blues watadai ada kubwa kwa beki huyo wa Timu ya Taifa ya England mwenye umri wa miaka 23. (*Teamtalk*)

### KELLY ANUKIA MILAN

AC Milan imeonyesha nia ya kumsajili beki raia wa England, Lloyd Kelly mwenye umri wa miaka 25 kutoka Bournemouth, ingawa Tottenham pia wanaonekana kumnyatia. (*Tuttosport*)

### KELLY AGOMBEWA ULAYA

KLABU za Juventus, Borussia Dortmund, Fulham na West Ham United ni miongoni mwa timu nyingine za Ulaya ambazo zimeonyesha nia ya kumhitaji, Lloyd Kelly ambaye mkataba wake unaisha msimu ujao. (*90 min*)

### VARMEEREN ANUKIA ARSENAL

ARSENAL huenda wakamnunua kiungo wa kati wa Royal Antwerp, Arthur Vermeeren kwa ada ya pauni milioni 13 ifikapo Januari, lakini Barcelona pia wanamtaka mchezaji huyo wa kimataifa wa Ubelgiji mwenye umri wa miaka 18. (*Sport*)

### ZIDANE ATAJWA UNITED

KLABU ya Manchester United inatafuta mbadala wa kocha Erik ten Hag, huku Kocha wa Sporting Lisbon, Ruben Amorim na mkufunzi wa zamani wa Real Madrid, Zinedine Zidane wakipigiwa upatu kuchukua nafasi yake. (*Times*)

### UNITED YASAKA STRAIKA

KLABU ya Manchester United inataka kumsajili mshambuliaji mwingine ili kumsaidia, Rasmus Hojlund huku wasiwasi ukiongezeka kuhusu maendeleo ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20. (*Mail*)

### TONEY KUTUA UNITED

IVAN Toney wa Brentford ni chaguo mojawapo linaloangaliwa na Kocha, Erik Ten Hag pamoja na mshambuliaji wa Napoli na Nigeria Victor Osimhen (24) na mshambuliaji wa Iran na Porto, Mehdi Taremi (31). (*Express*).

### CHALOBAH AITAJA DORTMUND

BEKI wa Chelsea na Timu ya Taifa ya England, Trevor Chalobah mwenye umri wa miaka 24, amevutiwa na vigogo wa Ujerumani, Borussia Dortmund. (*Sun*)

### MUBAMA AIGOMEA WEST

MSHAMBULIAJI wa Timu ya Taifa ya England, Divin Mubama mwenye umri wa miaka 19, amekataa kuongezewa mkataba katika wake na West Ham ikiwa imesalia muda wa mwaka mmoja katika mkataba wa sasa na klabu hiyo. (*The Athletic*)

### MADRID KUIKAMUA VILLA

ASTON Villa na West Ham wameambiwa na Real Madrid lazima walipe takribani euro milioni 20 kama wnamtaka huduma ya Brahim Diaz mwenye umri wa miaka 24. (*Birmingham*)

### CLARKE SOKONI RASMI

SUNDERLAND imeonyesha nia ya kumpeleka kwa mkopo winga wa Timu ya Taifa ya England, Jack Clarke mwenye umri wa miaka 22, kwa klabu nyingine. (*Sunderland Echo*)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# MADRID YAANIKA DAU KUMNASA VINICIUS JR

**Vigogo hao wa Hispania wasema ili kumng'oa klabuni hapo...**

**MADRID,** Hispania

ILI kumsajili Vinicius Jr kutoka Real Madrid, klabu inayomtaka itapaswa kulipa dau la euro bilioni moja.

Hatua hiyo imekuja baada ya Mbrazili huyo kumwaga wino kwenye mkataba mpya wa miaka minne ili kuendelea kukipiga kwa vigogo hao wa Hispania.

**90mins imeripoti, katika mkataba huo kuna kipengele kinachomruhusu nyota huyo kutimka Real Madrid kwa euro bilioni moja.**

Vinicius Jr alimwaga wino katika mkataba huo mapema wiki hii ili kuendelea kusalia kwa mabingwa hao mara 14 wa Ligi ya Mabingwa Ulaya, hadi mwaka 2027.

Winga huyo mwenye umri wa miaka 23, amefikia hatua hiyo baada ya majadiliano ya pande zote mbili kwa miezi kadhaa.

Vinicius alijiunga katika kikosi cha Real Madrid mwaka 2018, akitokea katika klabu ya Flamengo ya nchini Brazil.

Imeripotiwa Vinicius Jr na uongozi wa Real Madrid walifikia mwafaka wa dili hilo mapema mwaka huu, kabla ya mapema mwezi huu kukamilisha baadhi ya vipengele na kisha kutia saini.

Mkataba huo umemfanya Vinicius Jr kuwa miongoni mwa nyota wanaolipwa fedha nyingi katika klabu hiyo kutoka jiji la Madrid.

Ufundi wa kusakata soka, kasi na kufunga mabao kumemwezesha nyota huyo kuwa mmoja kati ya wachezaji bora duniani kwa miaka michache iliyopita.

Katika mashindano yote msimu uliopita, Mbrazili huyo alifungia Real Madrid mabao 23.

Katika Ligi Kuu ya Hispania msimu huu, nyota huyo amefunga mabao mawili na kutoa pasi moja ya bao katika michezo minane alipocheza.

# DAU LA TONEY LAPANDISHWA



**LONDON,** England

MABOSI wa Brentford wanataka pauni milioni 80 ili kumuuza mshambuliaji wao, Ivan Toney katika dirisha lijalo la majira ya baridi, ambapo vigogo wengi Ulaya wameonyesha nia ya kutaka kumsajili.

Licha ya Mshambuliaji huyo kutocheza tangu kuanza kwa msimu huu, huduma yake imekuwa ikimendewa na vigogo wengi ambao wamevutiwa na kiwango alichoonyesha msimu uliopita.

Arsenal ni moja ya timu zinazoonekana kuhitaji sana huduma yake, lakini huenda ikarudi nyuma kutokana na kiasi kikubwa cha fedha kinachohitajika na mabosi hao.

Awali ripoti zilidai Brentford ilihitaji pauni milioni 60 ili kumuuza nyota huyo lakini baada ya kuona kuna timu nyingi zenye uhitaji naye wameonekana kupandisha dau lake.

Toney ambaye ni mchezaji wa kimataifa wa England kwa sasa amefungiwa kucheza soka baada ya kukutwa na hatia ya kujihusisha na masuala ya kamari, mkataba wake unatarajiwa kumalizika mwaka 2025.

Msimu uliopita staa huyu alikuwa wa moto zaidi, alicheza mechi 35 za michuano yote, akafunga mabao 21 na kutoa asisti tano.

# Deschamps agoma kumpa 'maua' Messi

**PARIS,** Ufaransa

KOCHA Mkuu wa Ufaransa, Didier Deschamps amesema hawezi kukubali Lionel Messi ndiye mchezaji bora zaidi kuliko Cristiano Ronaldo na Kylian Mbappe.

Hiyo imekuja baada ya Messi kutangazwa mshindi wa Ballon d'Or kwa mara ya nane, akiwa ndiye kinara, huku Ronaldo akifuatia kwa kubeba tuzo hiyo mara tano, Mbappe bado hajafanikiwa kuibeba.

Mbappe ambaye alikuwa na kikosi cha Ufaransa katika michuano ya Kombe la Dunia 2022, alishuhidia wakipoteza mchezo wa fainali dhidi ya Argentina ya Messi.

Licha ya mafanikio ya Messi katika maisha yake ya soka, Deschamps amesema hadhani kama mshambuliaji huyo wa zamani wa Paris Saint-Germain anaweza kuchukuliwa kuwa bora zaidi wa wakati wote.

"Waargentina wanasema Messi ndiye bora zaidi wakati wote, lakini ni vigumu kusema Messi ni bora kuliko Cristiano Ronaldo au Kylian Mbappé," amesema Deschamps.

Katika tuzo za Ballon d'Or zilizotolewa mapema juma hili na Messi kushinda, Mbappé alishika nafasi ya tatu nyuma ya Erling Haaland wa Manchester City aliyemaliza kwenye nafasi ya pili.





# Klabu za Ulaya zamgombea Naj Razi

**LONDON,** England

KLABU za England, Arsenal na Chelsea zinapamnbana na Real Madrid ya Hispania ili kumsajili mchezaji chipukizi wa Ireland, Naj Razi.

Yosso huyo ameonekana na klabu kubwa za Ulaya baada ya kupangwa katika kikosi cha kwanza cha Shamrock Rovers FC msimu huu.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 17, amecheza mara tano kipindi hiki timu hiyo inayojulikana pia kama Hoops, ambayo inajiandaa kuikaribisha Sligo Rovers kwenye Uwanja wa Tallaght.

Na amekuwa na klabu hiyo tangu akiwa mtoto mdogo, alijiunga na shule ya timu hiyo akiwa na umri wa miaka saba.

Chipukizi huyo amewakilisha timu ya taifa ya Ireland ya wachezaji wenye umri chini ya miaka 17 tangu mwaka 2022 na hadi sasa amecheza mechi 14 na kufunga mabao manne na kusaidia kupatikana kwa magoli manne.

Alianza katika mashindano ya umri chini ya miaka 17 ya Ireland ambayo ilitolewa katika hatua ya robo fainali na Hispania baada ya kufanya vizuri katika hatua ya makundi.

HABARI MICHEZO

# CRDB KUPELEKA WATEJA 8 KUSHUHUDIA AFCON 2024

Na Mwandishi Wetu

BENKI ya CRDB kwa kushirikiana na Kampuni ya Visa inayoongoza katika mfumo wa malipo ya kidigitali imezindua kampeni ya 'Tisha na Tembocard Tukakiwashe AFCON' ambayo itapeleka wateja nane watakaofanya miamala mingi zaidi kushuhudia fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON 2024), zitakazofanyika Ivory Coast mwakani.

Kampeni hiyo ni sehemu ya juhudi zinazofanywa na CRDB kupunguza matumizi ya fedha taslimu na kuhamasisha matumizi ya mifumo ya kidigitali ilizinduliwa jijini Dar es Salaam jana na itadumu kwa miezi mitatu.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Gerson Msigwa ameipongeza CRDB na Kampuni ya Visa kwa kuanzisha kampeni hiyo aliyosema imekuja wakati mwafaka ambapo sio tu itasaidia kupunguza matumizi ya fedha taslimu bali itahamasisha michezo kwa Watanzania.

"Mwaka huu timu yetu ya Taifa (Taifa Stars), imefuzu kushiriki fainali za AFCON zitakazofanyika Ivory Coast, hivyo kampeni hii inatoa fursa kwa mashabiki kwenda kuishangilia. Nawapongeza sana CRDB na Kampuni ya Visa kuja na kampeni hii madhubuti ambayo itatoa fursa adhimu ya watu kushuhudia fainali za AFCON," alisema Msigwa.

Aliongeza pamoja na kampeni ya "Tisha na TemboCard Visa Tukakiwashe AFCON" kuhamasisha michezo, pia inaunga mkono juhudi za serikali katika kukuza uchumi wa kidigitali.

"Uchumi wa kidigitali unahitaji njia mpya za malipo ambazo hazimlazimu mtu kutembea na fedha taslimu. TemboCard Visa inarahisisha malipo hayo kupitia majukwaa tofauti ya ndani hata kimataifa," amesema.

Naye Ofisa Biashara wa CRDB, Boma Raballa alisema "Tunatambua upendo wa Watanzania walionao katika mpira wa miguu. Tunaamini kuwapa fursa hii ya kushuhudia fainali za AFCON 2024 kutawaongezea ladha isiyosahaulika."

Raballa amesema washindi naye watakaopata nafasi hiyo watachukuliwa miongoni mwa watumiaji wa TemboCard Visa watakaofanya miamala isiyopungua 30 kwa mwezi sawa na wastani wa muamala mmoja kila siku.

Salma Ingabire, Meneja Mkazi wa Visa Tanzania alisema "Kama mtoa huduma pekee wa huduma za malipo pekee wa TotalEnergies CAF AFCON, Visa tunafurahi kuingia ubia na CRDB ili kuwatuza wateja watakaobahatika kwa kuwapa nafasi ya kushuhudia timu bora za Afrika zikicheza.

Mbali na kushinda safari hiyo, wateja watakuwa na fursa ya kushinda zawadi nyingine ikiwamo seti ya sofa na vifaa vya kielektroniki mfano runinga na friji.

> **"Mwaka huu timu yetu ya Taifa (Taifa Stars), imefuzu kushiriki fainali za AFCON zitakazofanyika Ivory Coast,**

# *Mudathir, Fei Toto wanusurika kifungo*

Na Adam Fungamwango

WACHEZAJI Mudathir Yahya wa Yanga na Feisal Salum 'Fei Toto' kutoka Azam FC wametozwa faini ya Sh. milioni mbili kila mmoja kwa kosa la kukataa kupeana mikono na waamuzi wakati timu hizo zilipokutana katika mechi ya Ligi Kuu Bara iliyochezwa Oktoba 22, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Adhabu hiyo imetolewa na Kamati ya Uendeshaji na Usimamizi wa Ligi ya Bodi ya Ligi Kuu Tanzania (TPLB), iliyokutana Oktoba 30, mwaka huu ili kujadili mwenendo na matukio mbalimbali ya ligi hiyo inayoendelea nchini.

Mudathir na Fei Toto, wote ni wachezaji wa Timu ya Taifa ya Zanzibar (Zanzibar Heroes), ambapo sasa watalazimika kulipa faini hiyo kwa makosa waliyofanya katika mechi iliyomalizika kwa Yanga kushinda mabao 3-2.

Kamati imesema imetoa adhabu hiyo kwa kuzingatia kanuni ya 41:5 (5:4) ya Ligi Udhibiti wa wachezaji.

Hata hivyo adhabu hiyo inatofautiana na ile iliyotolewa Novemba, mwaka jana kwa Clatous Chama wa Simba na Stephane Aziz Ki ambao walifungiwa kucheza michezo mitatu na adhabu ya kulipa faini ya Sh. 500,000 kila mmoja kwa kosa la kukwepa kusalimiana na wachezaji wa timu pinzani katika mechi ya dabi iliyomalizika kwa sare ya bao 1-1.

Adhabu zao pia zilihukumiwa kwa kifungu kile kile cha 41:5 (5.4).

Taarifa iliyotolewa juzi jioni inasema pia imemwondoa katika orodha ya waamuzi kwa raundi tatu, mwamuzi msaidizi namba moja aliyesimamia mechi hiyo ya Yanga dhidi ya Azam, Janeth Balama kutoka Iringa kwa kosa la kushindwa kutafsiri vyema sheria za mpira wa miguu katika mchezo huo.

Kamati pia imemwadhibu straika wa Singida Fountain Gate, Habib Kyombo kwa kufanya vitendo vilivyoashiria ni imani za kishirikiana katika mchezo dhidi ya Namungo FC uliochezwa Oktoba 21, mwaka huu kwenye Uwanja wa Majaliwa, Lindi, timu yake ikishinda mabao 3-2.



Wachezaji wa Azam FC wakifanya mazoezi kwa ajili ya kujiandaa na mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Ihefu itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Highland Estates ulioko Mbarali, Mbeya. **PICHA: MTANDAO**

## Robertinho, Gamondi wauona ushindi 100%

INATOKA UK 24

kutengeneza tofauti katika msimamo wa ligi .

"Tunatakiwa kumaliza mbio za ubingwa mapema, kurahisisha kazi na kupunguza presha, tumeona Azam FC wameshajitoa kwenye mstari sasa tunataka kusaka ushindi mchezo wetu wa Jumapili.

Tayari wameshapoteza alama tatu na katika mchezo huu tunahitaji kupunguza tatu nyingine, wachezaji wanatambua umuhimu wa mchezo huu na kuhakikisha wanapambana kuwapa furaha mashabiki wetu," alisema Ahmed.

## Simba ni ugenini,

INATOKA UK 24

mawili tu, ikivuna jumla ya pointi 15, kati ya 18 ilizonazo mpaka sasa.

Katika mechi zake za nyumbani ilizichakaza KMC na JKT Tanzania mabao 5-0 kila moja, ikaifunga Namungo bao 1-0, ikashinda mabao 2-0 dhidi ya Singida Fountain Gate na ikaifunga Azam FC mabao 3-2.


Hata hivyo Yanga inaonyesha kuwa haijafanya vizuri sana ikicheza ugenini kwani katika mechi mbili ilizocheza imepoteza moja na kushinda moja.

Ilipokea kipigo cha mabao 2-1 dhidi ya Ihefu kwenye Uwanja wa Highland Estates, Mbeya mechi iliyochezwa Oktoba 4, na ikashinda mabao 3-0 dhidi ya Geita Gold, Uwanja wa CCM Kirumba Mwanza.

# Michezo

Jumamosi Novemba 4, 2023

Nipashe


Dau la Toney lapandishwa UK. 22

# Robertinho, Gamondi wauona ushindi 100%

## ●●● Baleke, Aziz Ki kubeba mikoba ya timu zao ili kuhakikisha pointi...

**Na Saada Akida**

PRESHA imeendelea kupanda na kushuka kuelekea mchezo wa watani wa jadi, Simba na Yanga utakaochezwa kesho kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, huku kila upande ukiwa na matumaini ya kuibuka na ushindi.

Hata hivyo, mshambuliaji wa Simba, Jean Baleke anaonekana ndiye mchezaji ambaye ana nafasi nzuri zaidi ya kuisaidia timu yake kuondoka na ushindi huku kwa upande wa Yanga, mikoba ikiachwa kwa Stephanie Aziz Ki.

**Baleke na Aziz Ki kila mmoja amefunga mabao 6, lakini Mkongomani wa Simba akitumia dakika chache uwanjani ukilinganisha na nyota huyo wa Yanga.**

Kuelekea mechi hiyo, Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi amesema mchezo huo utakuwa na ushindani mkubwa kutokana na namna alivyowasoma wapinzani wake ambao hivi karibuni walikuwa katika mashindano ya kimataifa ya African Footbal League.

Gamondi alisema anafahamu mechi hiyo haitakuwa nyepesi kwa kila upande kutokana na maandalizi ambayo wamefanya na ubora wa wachezaji waliokuwa nao.

Kocha huyo alisema watacheza na timu nzuri na yenye uzoefu wa michezo mikubwa, hivyo wamejiandaa kuonyesha mchezo mzuri na kwa lengo la kutafuta matokeo chanya.

Alisema wanawaheshimu Simba lakini anajua kila mmoja anahitaji kushinda ili kujiweka katika nafasi nzuri katika mbio za ubingwa wa msimu huu.

"Tunaenda kutafuta alama tatu, tumesahau matokeo ya mechi ya kwanza, ulikuwa mchezo wa mwanzo wa msimu, uwanja haukuwa mzuri kwa timu zote kushindwa kucheza soka la aina tunayocheza.

Lakini Jumapili (kesho) tunaenda kucheza kwenye uwanja mzuri, mchezo utakuwa mzuri sana kwa sababu utakuwa wa kimbinu na kiufundi, ni wazi kila mmoja anahitaji matokeo chanya," alisema Gamondi.

Naye beki wa Yanga, Ibrahim Hamad (Bacca), alisema wamejipanga vizuri na anayefanya vizuri katika dakika 90 ataondoka na alama tatu katika mchezo huo.

"Haitakuwa mechi rahisi na kila mmoja wetu anahitaji kupata alama muhimu, tunahitaji kuzitumia vizuri dakika 90, kupambana na kusaka ushindi. Tumeona ubora wa safu ya ushambuliaji wa wapinzani wetu na kama mabeki hatutakuwa tayari kuruhusu kufungwa kirahisi," alisema beki huyo.

Kwa upande wa Simba, Roberto Oliveira (Robertinho), amesema ameifanyia kazi safu yake ya ulinzi kwa lengo la kutofanya tena makosa yatakayowagharimu.

Robertinho aliweka wazi ameshabaini changamoto za safu yake ya ulinzi na amezifanyia kazi ili kutoruhusu mabao kirahisi katika kila mechi kama ilivyojitokeza kwenye michezo iliyopita.

"Tuna mechi ngumu sana mbele yetu, tumekuwa tukiruhusu mabao, tunapotangulia kupata ushindi, ukiangalia mechi ya Al Ahly zote mbili nyumbani na ugenini lakini mchezo wetu na Ihefu FC, tumeruhusu bao licha ya kushinda.

Wachezaji wangu wanatambua umuhimu wa mechi yetu ijayo na tunahitaji kupata matokeo mazuri, nafahamu ubora wa wapinzani wetu, jukumu langu kubwa ni kufanya kazi changamoto za kikosi changu," alisema Robertinho.

Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano Simba, Ahmed Ally amesema wamejiandaa vizuri na kikosi kipo imara kutafuta alama tatu ambazo zinaenda

INAENDELEA UK 23




Aziz KI

Baleke

## Simba ni ugenini, Yanga nyumbani

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI mafahari wawili wa soka la Tanzania wanatarajia kukutana katika mechi ya mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu Bara itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, Simba inaonekana hatari zaidi wakicheza ugenini wakati Yanga ni moto wakiwa nyumbani.

Kwa maana hiyo, makocha wa pande zote mbili, Roberto Oliveira wa Simba na Miguel Gamondi wa Yanga watakuwa na kazi nzito ya kuhakikisha wanarekebisha makosa au mapungufu katika vikosi vyao ili hali hiyo isitokee kwenye mechi ya kesho.

Gamondi atakuwa na kazi ya kuhakikisha timu yake haiendelei kuwa mnyonge ikicheza ugenini huku Robertinho akiwa na kazi ya kurekebisha mapungufu yanayoifanya timu hiyo isiwe na takwimu nzuri zaidi inapopeperusha bendera yake nyumbani.

Kumbuka Simba ndiyo itakuwa mwenyeji wa mechi hiyo, Yanga ikiwa mgeni kikanuni, hivyo takwimu haizibebi vyema timu zote mbili kwenye mechi hiyo.

Kwa mujibu wa takwimu kutoka dawati la michezo la Nipashe, Simba imecheza mechi sita za Ligi Kuu mpaka sasa, imeshinda mechi tatu ugenini ikiwa imevuna pointi tisa ikishinda zote, ikifunga mabao tisa ambayo ni mengi kuliko iliyoyafunga ikicheza uwanja wake wa nyumbani.

Simba imefunga mabao saba tu ikicheza kwenye viwanja vya Benjamin Mkapa na Uhuru, haijapoteza mechi yoyote ugenini ikizifunga Mtibwa Sugar mabao 4-2, Prisons mabao 3-1 na Singida Fountain Gate mabao 2-1.

Pamoja na Simba haijapoteza mechi mechi yoyote ikicheza nyumbani, lakini rekodi zinaonyesha ugenini ndiyo imefanya vizuri, ikifunga magoli mengi zaidi na ikishinda kwa asilimia 100 kuliko wapinzani wao Yanga.

Kwa upande wa mahasimu wao wa jadi Yanga, takwimu zinaonyesha nguvu yao kubwa ni kwenye uwanja wa nyumbani, Benjamin Mkapa na Azam Compex, Dar es Salaam.

Timu hiyo imeshinda mechi zote tano ilizocheza nyumbani, ikifunga mabao 16 na kuruhusu

INAENDELEA UK 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002